

Ni Kuchomoza Kwa Jua



Na tuinamishe vichwa vyetu. Bwana, tunapokusanyika hapa asubuhi hii njema ya Pasaka, tunaona chipukizi ndogo zikichipua, nyuki wakiruka na kuingia mle wakapata riziki yao, ndege wakiimba kama kwamba mioyo yao itapasuka kwa shangwe, kwa sababu kuna Pasaka fulani. Tunaamini ya kwamba ulimfufua Yesu katika wafu, miaka mingi iliyopita, leo, nasi tunaisherehekea siku hii ya ukumbusho.

² Pasaka na ije miongoni mwetu sisi sote, leo. Tujalie sisi, kama watumishi Wake, kulifahamu Neno Lake, ya kwamba tulikuwa katika ushirika Wake wakati huo, na ya kwamba sasa tumefufuka pamoja Naye na tunaketi pamoja katika ulimwengu wa Roho.

³ Ibariki ibada hapa Maskanini, na kote nchini ambapo inaenda, kwa simu hii.

⁴ Waponye wagonjwa wote na wanaoteseka. Na iwe Pasaka kwa ajili yao, pia, na kutoka katika magonjwa wapate nguvu. Na hao waliokufa katika dhambi na maovu, na waishi leo kwa njia ya Kristo. Nasi tutakusifu Wewe, kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

⁵ Hakika nahesabu haya kuwa ni majaliwa ya ajabu sana, asubuhi ya leo kurudi tena hapa Jeffersonville, Indiana, kuwa pamoja na kusanyiko hili kuu, kanisa limejaa kabisa na wanasimama, na kando-kando na huko nje, na mahali pa kuegeshea magari na kila mahali. Kwenu ninyi watu kwenye simu na kote nchini, ni asubuhi ya kupendeza sana hapa.

⁶ Saa kumi na moja asubuhi ya leo, rafiki yangu mdogo mwenye kifua chekundu aliruka dirishani akaniamsha. Ilionekana kana kwamba moyo wake mdogo ungepasuka, akisema, “Amefufuka.” Daima nimewazia juu ya ndege huyu mdogo kuwa ni rafiki yangu, kwa maana nampenda.

⁷ Kama vile hadithi kumhusu yeye inavyosema, “Ndege mdogo wa hudhurungi alimwona Yeye akiteseka msalabani, ambapo dhambi ilikuwa imemweka.” Bila shaka, maskini ndege huyo hakuwa na dhambi. Haikumbidi Yeye kufa kwa ajili ya maskini ndege huyo. “Bali aliruka akaenda msalabani na kujaribu kuitoa ile misumari, kwa midomo yake midogo, ndipo akafanya kifua chake chote kuwa chekundu.” Na hivyo ndivyo ninavyotaka changu, pia, kama ngao, ya kujaribu kukinga Jambo hili tukufu ambalo alilifia.

⁸ Tukitambua ya kwamba wakati wetu ni mdogo hapa, hasa kwa hao marafiki wanaosikiliza kwa simu asubuhi hii,

ningetaka kuelekeza macho yenu asubuhi ya leo kwe—kwenye picha ile ambayo wakati fulani uliopita ilipigwa na kamera, ya ono nililokuwa nimeona hapa Maskanini, la kuhama Indiana, kwenda Arizona; ambapo ilikuwa nikutane, katika mfano wa piramidi, na Malaika saba. Bila kujua ambalo lingetukia baadaye, nilipofika kule, nikifikiri ilikuwa ndio mwisho wa maisha yangu, ya kwamba hakuna mtu angaliweza kuustahimili mlipuko huo; nami nina hakika ninyi nyote mnakifahamu kisa hicho. Halafu tena kwenye yale Magenge ya Sabino, asubuhi moja kama hii, nilipokuwa katika maombi, kulikuweko na upanga uliowekwa katika mkono wangu, na kusema, “Hili ni Neno, na Upanga wa Neno.”

⁹ Baadaye, wale Malaika walitokea kama ilivyotabiriwa. Na wakati uo huo, kikundi kikubwa cha Mianga kikaondoka mahali nilipokuwa nimesimama, na kupanda juu maili thelathini hewani, na kufanya duara, kama mabawa ya wale Malaika, na kuchora angani mfano wa piramidi katika kundi lile lile la Malaika lililotokea.

¹⁰ Sayansi ilipiga picha hiyo, kote kote kutoka Mexico, ilipokuwa inasogea kutoka Arizona ya kaskazini, ambako Roho Mtakatifu alisema ningekuwa nimesimama, “maili arobaini kaskazini-mashariki mwa Tucson.” Kisha ikapaa hewani, na gazeti la *Life* lilichapisha hizo picha, “Kitu fulani kisichoelezeka juu sana hewani, ambako hakungeweza kuwa na unyevu, ambako hakungeweza kuwa na mivuke ya kitu cho chote; maili thelathini kwenda juu, na maili ishirini na saba kutoka upande mmoja hadi mwingine,” na ikipanda juu moja kwa moja kutoka walipokuwepo wale Malaika.

¹¹ Sasa, waliulizauliza, wapate kujua. Sayansi, mmoja wao huko Tucson, alitaka kujua ina maana gani, bali mimi sikuwaambia. Ninyi nyote mlijua jambo hilo, lilikuwa limesimuliwa hapo awali. Bali halikuwa kwa ajili yao; lilikuwa kwa ajili yenu.

¹² Na kwa hiyo Yeye alinena nami hapo, akasema, “Zile Muhuri Saba zitafunguliwa. Zile siri saba, ile siri yenye sehemu saba ya Biblia, ambayo imefungwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, itafunuliwa.” Nasi, tukali tu kundi dogo nyenyekevu, tukilinganishwa na ulimwengu wote, tumezifurahia baraka hizi, kuzisikiliza hizo siri. *Ndoa, talaka, uzao wa nyoka*, maswali haya yote mbalimbali, yamekwisha kufunuliwa kwetu kabisa, si na mwanadamu, bali na Mungu, Mwenyewe, ambaye amezifungua hizo siri saba; juu ya kile Kanisa lilichokuwa, jinsi lilivyokuwa katika Kristo hapo mwanzo, na jinsi litakavyofunuliwa katika siku ya mwisho.

¹³ Na sasa, hili lilipokuwa linapaa juu, tuna hiyo picha huko nje kwenye ubao. Lakini, basi, nina picha iliyopo hapa, kama

mkiangalia, kama ilivyokuwa katika gazeti la *Life*. Bali sijui kama wasikilizaji wangu, wanaoonekana hapa, wamepata kweli kuiangalia picha hii, mnaona, mnaona, inavyopasa.

¹⁴ Mnakumbuka, nilikuwa ninahubiri wakati ono hili lilipokuja, juu ya somo la Kitabu cha Ufunuo, ambapo mahakimu wa kale, ambapo tunamwona Yesu katika Ufunuo 1. Tulipoanza kuzifungua zile Muhuri Saba . . . ama zile—ama zile Nyakati za Kanisa, hasa, kabla tu ya kufunguliwa kwa zile Muhuri Saba. Kristo alikuwa amesimama akiwa na “nywele kama sufi, nyeupe.” Nami nikawasimulia jambo hilo, ya kwamba mahakimu wa kale wa Kiingereza, na mahakimu wa zamani za kale, walipoenda mahakamani, kuapishwa, walipewa mamlaka yao kuu. Walivaa wigi nyeupe, kama ilivyokuwa, juu ya vichwa vyao, kuonyesha mamlaka yao kuu.

¹⁵ Vema, kama utaigeuza hiyo picha namna *hii* na uangalie, labda waweza ukaiona kutoka kwa wasikilizaji, ni Kristo. Angalieni macho Yake yakiangalia *hapa*, kikamilifu tu iwezavyo kuwa; amevaa ile wigi nyeupe ya Uungu Mkuu na Hakimu wa mbingu zote na nchi. Je! mnaweza kuyaona macho Yake, pua, Kinywa Chake? [Kusanyiko, “Amina.”] Igeuzeni tu picha kutoka upande *huu*, jinsi walivyokuwa wamefanya; upande *huu*, jinsi inavyopaswa kuwa. Nanyi. . . Mnaweza kuiona? [“Amina.”—Mh.] Yeye ndiye Hakimu Mkuu. Hakuna mwingine ila Yeye. Na huo ni utambulisho mkamilifu tena, thibitisho ya kwamba Ujumbe huu ni Kweli. Hii ndiyo ile Kweli. Ni Kweli. Na kumfanya Yeye si nafsi ya tatu, bali Nafsi pekee!

¹⁶ Akiwa na nyeupe, mnaona, mnaona weusi, uso Wake, ndevu Zake, na macho Yake. Pia angalieni, Yeye anaangalia. . . Kutoka Kwake inakuja Nuru hii inayoangaza upande wa kuume, ambako anaangalia. Na msalabani, huko ndiko alikoangalia, upande wa kulia, ambako alimsamehe yule mwenye dhambi. Katika Nuru ya kufufuka Kwake, tungali tunasonga mbele katika Jina Lake.

¹⁷ Ningetaka, asubuhi ya leo, kwamba ningalikuwa tu na wakati mwingi wa ku—kutumia juu ya matukio haya ya ajabu ambayo bila shaka kabisa, yamethibitishwa kwa miaka thelathini iliyopita, ama miaka thelathini na mitano, papa hapa kwenye kanisa hili; tangu kule chini mtoni, wakati Nuru ile ile iliposhuka chini hapa Jeffersonville, katika mwaka wa 1933, na kunena maneno hayo, “Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia kwa pili.” Tuko katika wakati wa mwisho, nasi tunaona jambo hilo. Mara kwa mara tunashangaa kwa nini haujasambaa kote duniani; labda wakati mwingine tutapata wakati wa kueleza jambo hilo, Mungu akipenda.

¹⁸ Sasa nawatakeni mfungue ka—katika Biblia zenu, kama tunavyoamini daima ya kwamba Neno halina budi kutangulia,

kusomwa kwa Neno. Daima mimi hulisoma Hilo, kwa maana Hilo. . . Maneno yangu ni neno la mwanadamu, litashindwa; bali Neno la Mungu haliwezi kushindwa kamwe.

¹⁹ Sasa tu—tutasoma kutoka kwenye Maandiko Matakatiifu, somo fulani. Nasi tunawatakeni mfungue, kwanza, kutoka kwenye sehemu tatu katika Biblia, ambazo nimechagua kusoma. Moja ya hizo iko katika Ufunuo, sura ya 1, na aya ya 17 na 18; hapa ndipo alipotokea na “nywele Zake nyeupe kama sufu; na miguu Yake ilikuwa kama shaba.” Na halafu nawatakeni pia mfungue, katika Biblia zenu, Warumi 8:11. Nimechagua, asubuhi ya leo, mahali patatu pa kusoma, kutoka kwenye Maandiko Matakatiifu, kwa ajili ya Ujumbe wangu leo, ambao Bwana ameweka moyoni mwangu kwa ajili ya kufufuka. Halafu nawatakeni mfungue, pia, Marko 16:1 na 2. Humo nitatoa fungu la—langu la maneno.

²⁰ Sasa katika Ufunuo 1:18, tunasoma maneno haya, 17 na 18:

Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho,

Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Amina. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu..”

²¹ Na katika Warumi sura 8 na aya ya 11, tunasoma haya:

Lakini, ikiwa Roho wake yeye aliyemfufua. . . Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo. . . katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.

²² Na sasa katika Marko sura ya 16, ile sura ya kufufuka, sura ya 16, aya ya 1 na ya 2.

Hata sabato ilipokwisha kupita, Mariamu Magdalene mamaye. . . na Mariamu mamaye Yakobo, na Salome walinunua manukato wapate kwenda kumpaka.

Hata alfajiri mapema, siku ya kwanza ya juma, wakaenda kaburini, jua lilipoanza kuchomoza;

²³ Sasa, somo langu asubuhi ya leo, nataka kuchukua somo: *Ni Kuchomoza Kwa Jua.* Na kichwa cha somo, nataka kutumia, “nguvu za Kuhuisha.”

²⁴ Sasa, mnajua, labda mmekuwa mkisikiliza redio na wahudumu mbalimbali wakizungumza. Na Ndugu yetu mwema Neville asubuhi ya leo akizungumza juu ya somo lake la Pasaka, juu ya Ufufuo. Nami nilifikiri labda ningelilichukulia njia tofauti ki—kidogo, si kwamba niwe tofauti, bali kuongezea kitu kidogo zaidi, labda katika upande

mwingine, kwa ajili yenu. Maandiko, kila upande unaoendea kwenye Maandiko, hayo kila mara humtangaza Yesu Kristo. Huwezi kuliepuka jambo hilo, kwa njia yo yote. Daima yanamtangaza Yeye.

²⁵ Sasa, wakati ulimwengu leo katika ibada ya—ya ukumbusho, ama, tuseme, angaa Marekani na sehemu hii ya dunia, asubuhi ya leo, katika makanisa na kila mahali, wanasherehekea kumbukumbu la—la ushindi mkuu sana kuliko ushindi aliopata kuwa nao mwanadamu.

²⁶ Nafikiri, kama Mwokozi wakati alipokufa, ama kama mtoto mchanga wakati Yeye alipozaliwa, Yeye asingalikuwa hapa pasipo kuja duniani. Na wakati alipokufa, bila shaka Yeye alifanya upatanisho kwa ajili ya dhambi yetu. Lakini, hata hivyo, kumekuweko na watoto wengi wazuri na wachanga waliozaliwa, na kumekuwa na watu wengi ambao wameteseka na kufa kwa ajili ya kusudi halisi, bali hapajakuweko na mmoja ambaye angaliweza kujifufua tena mpaka siku hii.

²⁷ Sasa, hilo ndilo juma lililo kuu sana katika historia, sherehe kuu sana ya wakati wote, Pasaka hii ndipo ambapo Yeye alithibitisha aliyokuwa amesema. Mwanadamu anaweza kusema mambo, bali hayawezi hasa kuaminiwa, kabisa, mpaka yatakapothibitishwa kuwa ni Kweli. Na kama Mungu, Ambaye alisema, “Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema,” Yeye asingeweza kuwaambia mfanye jambo ambalo asingeweza kufanya Yeye Mwenyewe. Kwa hiyo Yeye alithibitisha Huyu alikuwa ni nani aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu.

²⁸ Na, sasa, hii si siku ya ukumbusho tu, wa haya maua yote mazuri ya Pasaka, na kofia za Pasaka, na sungura wa pinki, na kadhalika, ambayo tumeingilia, na sherehe takatifu; ambazo ni sawa, bali hili silo jambo halisi kwa njia hiyo.

²⁹ Kama vile watu siku hizi wanavyojaribu kusema, “Inatupasa kutawadhana miguu mara moja kwa mwaka, Al—Alhamisi, na Ijumaa inatupasa kufanya ushirika,” na mafundisho yote mbalimbali ya... Wao wanabishana kama inapaswa kuwa siku *hii* ama siku *ile*, ama kama inapaswa kuwa siku ya Sabato ama siku ya kwanza ya juma; ama... Mambo haya yote ni mapokeo tu. Yatakufaa nini yo yote ya hayo, kwamba ulikuwa na Kwaresma ama hukuwa na Kwaresima, iwapo hamna Uhai ndani yako? Ni kumbukumbu tu. Ambayo, hamna kitu dhidi yake, bali bila shaka wao wametekeleza mapokeo yao, lakini wakaliacha jambo lililo muhimu.

³⁰ Shetani hajali wewe ni wa dini namna gani, ama jinsi uko sahihi katika Mafundisho yako. Kama ukikosa huo Uzima, wewe hutafufuka, kwa vyo vyote. Hata uwe wa dini jinsi gani,

uwe mwema jinsi gani, umekuwa ama utakuwa mfuasi wa makanisa mangapi, haijalishi hata kidogo isipokuwa umezaliwa mara ya pili.

³¹ Kwa hiyo, kama Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu, je! Yeye alimfufua kwa ajili ya ukumbusho? Na je! asubuhi hii ya ufufuo ni si—siku moja tu katika mwaka, ama siku fulani ambayo sisi husherehekea jambo hili? Ama, sisi ni wafadhiliwa wa kufufuka Kwake? Hii ina maana gani kwangu? Ina maana gani kwako? Sasa tunaamini, kwa imani, ya kwamba Yeye alifufuka katika wafu, lakini jambo hilo linanihusuje? Hiyo ilikuwa miaka elfu mbili iliyopita.

Sasa kupata somo hili!

³² Kwa vile nilikuwa nimechoka, mkono wangu ukiniuma, kutokana na sindano alizonindunga yule nesi. Kwa kuwa, tunaondoka kwenda nchi za ng'ambo sasa, kama mjuavyo, mnamo siku chache, nami sina budi kudungwa sindano hizi, mimi na mwanangu. Pamoja na kipindupindu, homa ya manjano, na kila kitu, nilikuwa nimechoka sana, zikinifanya niugue. Ambapo, Kaisari anakutaka udungwe sindano hizi kabla ya kuingia katika taifa lingine. Naye alisema, "Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, lakini basi mpeni Mungu yaliyo ya Mungu."

³³ Nami nilipokuwa nimeketi kule, nikishangaa ningewahubiri nini wasikilizaji hawa wanaongoja asubuhi ya leo; ambao ninashukuru sana kwa ajili yao, na wanaume na wanawake ambao wangeweza kuyahatarisha maisha yao kwa ajili ya yale ungelisema. "Nifanye namna gani? Nichukue somo gani?"

³⁴ Halafu basi wakati nilipokuwa nimeketi hapo, karibu kusinzia, mlango wangu ukapiga makelele, huko nje upande wa mbele wa nyumba. Kukiwa hakuna mtu ila mimi mwenyewe, kadiri nilivyojua mimi. Nikasikiliza. Sikusikia vizuri. Baada ya kitambo kidogo, mlango wa chumba cha faragha, ambacho nimekigeuza kuwa chumba changu cha kusomea, kulikuwa na makelele, na mtu fulani anakazana kuutikisa mlango. Nami ni—nikaenda mlangoni na kuufungua mlango, ndipo, ajabu hii, ma—maskini msichana anayependeza mwenye nywele za manjano na macho ya buluu amesimama pale, alionekana kama ua dogo la Pasaka; ambaye ameketi hapa akiniangalia sasa.

³⁵ Akanipa kadi. Nayo ilikuwa...Bila shaka, nafikiri nitakapofika nyumbani kutakuweko na kadi za Pasaka, na kadhalika; lakini ndiyo ya pekee, tangu nilipoondoka nyumbani, ambayo nilikuwa nimepokea. Ndipo akasema, "Ndugu Branham, hii imetoka kwangu mimi na kwa babangu." Alitaka kuwa na hakika ya kwamba "mimi" ilikuwa ndani yake. Na baba yake mwenye yabisi kavu,

anayeketi kwenye kiti cha kusukumia wagonjwa, alikuwa ameituma kadi hii. Nilipoichukua na kumshukuru maskini kipenzi huyo, hapo alipogeuka na kuondoka mlangoni, nilifungua ile kadi.

³⁶ Na kutoka kwenye kadi hii nikachukua somo langu. Kwa kuwa, kwenye hiyo kadi kulikuwemo na Marko Mtakatifu 16:1 na 2, jua limechomoza, jua lilikuwa linachomoza. Ndipo nikawaza juu ya jambo hilo, na ndipo somo la “kuhuishwa,” kwa Yesu Kristo kufufuliwa katika wafu, nikatoa somo langu.

³⁷ Sasa, jua, kwenye kuchomoza kwa jua. Vema, kulikuweko na wakati ambapo ulimwengu ulikuwa umo katika giza tupu. Ulikuwa ukiwa, tena mtupu. Nao wote ulikuwa umefunikwa na maji, na ulikuwa pale katika mazingira yenye giza, ukiwa, na utusitusi. Nayo Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji, na kusema, “Iwe nuru.” Mungu alikuwa na sababu ya kufanya jambo hilo, kwa maana kule chini ya maji hayo kulikuwemo na mbegu alizokuwa amepanda, nazo zilihita hiyo nuru ya jua zipate kuishi.

³⁸ Basi Nuru ya kwanza iliyopata kutolewa duniani ilikuwa Neno la Mungu lililonenwa. Nuru ya kwanza iliyopata kuigusa nchi ilikuwa Neno la Mungu lililonenwa. Yeye alisema, “Iwe nuru,” ikawa nuru. Hiyo iligeuza giza kuwa nuru kusudi itoe uumbaji wa shangwe na uhai juu ya nchi. Ndipo, Roho wa Mungu, alipokuwa anasogea kwa upendo na huruma, kwenye hiyo sikukuu, siku ya kwanza ya mwanzo wa uumbaji juu ya nchi; jua lilichomoza na kuangaza kote, miali yake, na kukausha maji kutoka ardhini, na kufanya anga la juu. Na, kwa mara yake ya kwanza, lilikuwa lilete shangwe na uhai duniani, kwa njia ya mbegu. Hiyo ilikuwa ni saa muhimu sana.

³⁹ Lakini, loo, haikuwa kitu, nuru hiyo ya jua, kama ile nuru ya jua kwenye ile asubuhi ya Pasaka. Wakati huu, huku jua likiruka angani, ilisababisha kuchomoza kukuu zaidi kwa jua kuliko ilivyowahi kuwa; kwa maana habari kuu zaidi ziliambatana na kuchomoza huku kwa jua, kuliko ilivyofanya katika kule kuchomoza kwa jua pale mwanzoni. Kuchomoza huku kwa jua kulileta habari, ya kwamba, “Yeye amefufuka! Amehuishwa katika wafu, kama alivyoahidi. Amefufuka katika wafu.”

⁴⁰ Mara ya kwanza jua lilipochomoza, katika Mwanzo, lilikuwa likileta ujumbe ya kwamba kutakuweco na uhai juu ya nchi, uhai upatikanao na mauti.

⁴¹ Lakini wakati huu, jua lilipochomoza, kulikuwa na kuchomoza ma—maradufu kwa jua; Mwana, mwingine, akifufuka. Ilikuwa ninii. . . si kuchomoza tu kwa j-u-a, ilikuwa ni M-w-a-n-a amefufuka kuleta Uzima wa Milele kwa Uzao wote ulioahidiwa wa Mungu ambao kwa kujua tangu zamani Yeye alikuwa ameuona ukiwa juu ya nchi.

⁴² Haikuwezekana tena u—uhai wa mimea kuishi kule nyuma hapo mwanzo bila j-u-a kuufanya hai; wala tena, leo, wakati wana wa Mungu wako juu ya nchi, inatakiwa Nuru ya M-w-a-n-a kuwaleta kwenye Uzima wa Milele. Wateule Wake ambao aliwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alikuwa amewachagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

⁴³ Na kwenye ile asubuhi ya Pasaka, basi, katika vumbi hili mahali fulani ilikaa miili yetu wakati huo, kwa maana sisi ni mavumbi ya dunia. Na huko Mbinguni kulikuwa na kitabu cha kumbukumbu, na sifa Zake zilikuwa ndani Yake, wakijua ya kwamba kwa kuwa huyu Mwana wa Mungu alifufuka, Hiyo pia ingemfufua awe Hai kila mwana ambaye alichaguliwa tangu zamani kwa ajili ya wakati huu mkuu. Yeye alijua ingekuwa hivyo. Basi huko kulikuwa kuchomoza kwa jua kwenye utukufu zaidi jinsi gani kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo, wakati kulipopambazuka kwanza.

Sasa, kwenye kuvunjwa huku kutukufu kwa ile Muhuri ya Pasaka!

⁴⁴ Sasa, leo tuna muhuri ya Pasaka ya kifua kikuu. Watu kupelekeana ujumbe, mmoja kwa mwingine, na kuunga mkono akiba hii kuu ama mradi, kwa ajili ya madaktari na sayansi ya madawa wapate kufanya jambo fulani, kuzuia ama kusaidia kifua kikuu. Hizo ni muhuri, kile tunachoita muhuri ya Pasaka, wakati tunapopelekeana ujumbe sisi kwa sisi. Bali tunapopokea huo ujumbe, hiyo muhuri inavunjwa, kwa maana muhuri ndiyo imeufungia huo ujumbe mle ndani.

⁴⁵ Na sasa, Muhuri ya kweli ya Pasaka, katika kuchomoza huku kwa jua, ilivunjwa; na ile siri, ya Uzima baada ya mauti; ilifunuliwa. Kabla ya wakati huo, hatukujua. Ulimwengu ulitutusa gizani, ukatutusa kila mahali, mwanadamu... mashaka. Nadharia zilikuwa miongoni mwa mioyo ya wanadamu, mapokeo yaliyobuniwa. Mwanadamu aliabudu sanamu. Waliabudu jua. Waliabudu miungu ya kila namna. Na watu wa kila namna waliotoa madai, wote walikwenda kaburini, nao wakakaa makaburini.

⁴⁶ Bali ile Muhuri ya kweli ilikuwa imekwishavunjwa, na Mtu Mmoja Ambaye wakati mmoja aliishi kama tunavyoishi sisi, akafa kama tutakavyokufa, alifufuka katika wafu. Ni asubuhi ya jinsi gani! Hakujapata kuwa na moja kama hiyo, katika historia yote ya ulimwengu. Ile siri ilifanywa wazi ya kwamba Yeye alikuwa Ufufuo na Uzima pia.

⁴⁷ Ndipo akasema, alipofufuka asubuhi hiyo, “Kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.” Yeye hakuwa tu mfadhili wa ule ufufuo, bali Wazao hao wote waliokuwa wakipumzika katika ahadi kuu ya Mungu walikuwa wafadhiliwa wa ufufuo huo wa Uzima. Kwa maana, Yeye

alisema, “Kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.” Huko kulikuwa kuvunjwa kwa ile Muhuri. Kwa kuwa alifufuliwa, vivyo hivyo kila mmoja aliye katika Kristo atafufuliwa pamoja Naye.

⁴⁸ Katika kuchomoza huku kwenye utukufu kwa jua, Mungu alikuwa amehakikisha, ama amethibitisha, Neno Lake. Utusitusi wote na mashaka yaliyokuwa yameingia kwenye mioyo ya watu yaliondolewa, kwa maana hapa alikuwako Yeye Ambaye siku moja alikuwa hai, akala, akanywa, na kufanya ushirika na binadamu, ambaye alisema, “Ninao uweza wa kuutoa uhai Wangu; na ninao uweza wa kuutwaa tena.” Na sasa si kwamba tu Yeye alikuwa ametoa tamshi hilo, bali alilithibitisha kuwa ni Kweli. Loo, hilo ni jambo lenye utukufu jinsi gani!

⁴⁹ Nina hakika asubuhi ya leo ya kwamba hata sisi, tunaoamini jambo hilo, hatuwezi kuelewa jinsi jambo hilo lilivyokuwa kuu. Kwa maana Yeye alifufuka katika wafu, sisi pia tayari tumefufuka katika wafu, kwa kuwa tulikuwa katika Yeye.

⁵⁰ Angalia sasa. Wakati utusitusi ulipokuwa umeifunika nchi, na hizo mbegu hazingaliweza kuishi bila j-u-a kuchomoza, na utusitusi ulikuwa umeifunika nchi. Na sasa M-w-a-n-a alikuwa amefufuka, na utusitusi wote ulikuwa umetoweshwa na Nuru hii, wakati ilipokuwa inasambaa kote katika mataifa, kwa watu, ya kwamba, “Hayupo hapa, bali Yeye amefufuka!” Ni—ni tamshi la jinsi gani! Yeye alikuwa amelithibitisha Neno Lake. Yeye alikuwa amelithibitisha kuwa—kuwa ni kweli, kwa kuwa alikuwa sasa ameshinda mauti, kuzimu, na kaburi.

⁵¹ Ule utatu wa ibilisi; mauti, kuzimu, na kaburi; kwa kuwa Shetani ndiye mwanzilishi wa mauti, yeye ndiye anayekumiliki kuzimu, na pia kaburi. Na huo ulikuwa ndio utatu wa Shetani, ukisababishwa na kitu kimoja, hicho kilikuwa mauti. Mauti, wewe unaingia kaburini; na kwa kuwa wewe ni mwenye dhambi, unaenda kuzimuni. Yote ni jambo moja, utatu wa Shetani, ambao ulikuwa ni mauti. Ambayo yalikuwa yamemshika mwanadamu mateka miaka hii yote.

⁵² Bali sasa ule utatu wa kweli wa Mungu, ukiwa Ndio uliodhihirishwa katika Kristo, Ambaye alikuwa Uzima, naye alikuwa ameivunja Mihuri na kumshinda adui, kisha akafufuka, akiwa Mungu Mmoja wa Kweli na aliye Hai. “Mimi ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai milele na milele, Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu.” Mungu, katika Mmoja, alifanyika Mwanadamu, akaishi miongoni mwetu, na akashinda kila adui. Na alikuwa amethibitisha ya kwamba utatu wa Shetani ulikuwa umeshindwa, na ya kwamba utatu wa Mungu ulikuwa umefunuliwa, maana ni Mungu peke Yake aliyekuwa na uweza wa kuurudisha uhai tena. Yeye alikuwa yule Imanueli. Mungu alikuwa amedhihirishwa katika mwili.

⁵³ Si ajabu Yeye angaliweza kudai pale, Mathayo sura ya 27, “Mamlaka yote Mbinguni na duniani nimepewa mkononi Mwangu. Mimi nawatuma mkawe mashahidi Wangu, kote duniani.” Yeye alikuwa ameshinda mauti, kuzimu, na kaburi pia. Si kwamba tu Yeye alifanya jambo hilo; na akatokea, akiwa mshindi, pamoja na mamlaka yote mbinguni na duniani. Yote aliyokuwa Baba, yote aliyokuwa Roho Mtakatifu, na yote yaliyopata kuweko, yalikuwa ndani Yake. “Nimepewa mamlaka yote Mbinguni na duniani.” Kitu kingine cho chote hakina nguvu. Yeye alikuwa amekishinda.

⁵⁴ Sasa! Halafu basi, si hayo tu, Yeye alituma Neno kwa wanafunzi Wake, wanaoamini. “Msiogope, kwa kuwa Mimi ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai tena milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu; tayari nimeyashinda. Msiogope tena, kwa maana kila Mzao aliyeamriwa na kuchaguliwa tangu zamani na Mungu atafufuka wakati Nuru hiyo itakaposambaa duniani, ya Injili yenye utukufu. Katika kila wakati, itazaa mazao ambayo Mungu aliyaamuru kufanya.” Yeye alikuwa amefufuka katika wafu.

⁵⁵ Lo, hilo ni jambo la ajabu jinsi gani, “Mimi ni hai, ama nimehuishwa.” Neno hilo linamaanisha, neno *kuhuishwa*, hilo neno la Kiyunani linamaanisha hicho ni “kitu kilichofanywa hai baada ya kufa.”

⁵⁶ Kama ile mbe—mbegu inayoingia ardhini, haina budi kufa, kila sehemu ya mbegu hiyo. Haina budi kuoza, kila sehemu ya hiyo mbegu. Na kila sehemu ya uhai, uliokuwemo katika hiyo mbegu, hauna budi kutokeza tena.

⁵⁷ Yeye “alihuishwa.” Si hilo tu. “Nami nitautuma Uhai ule ule ulionihuisha, zile Nguvu zilizozifufua kutoka kaburini, Mimi nitazituma kwenu, kuwahuisha, ili niliko nanyi mweko pia.”

⁵⁸ Katika Luka, sura ya 24, aya ya 49. Yeye alisema, “Tazama, nawaletae juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini kaeni, ama ngojeni, mjini Yerusalemu, hata mtakapovikwa uwezo utokao Juu.” Kuonyesha ya kwamba si kwamba tu Yeye alitwaa baraka zote toka kwenye jambo hilo, bali Yeye alishiriki baraka hizo.

⁵⁹ Yeye alikuja kukomboa, ama kufanya Hai, Uzao huo uliochaguliwa tangu zamani ambao Mungu aliuona kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu na akayaweka majina yao katika Kitabu cha Uzima. Nao hawa hapa duniani, bila tumaini; Yeye alikuja si kwamba tu awe hiyo Baraka, bali kushiriki hiyo Baraka na kila Mzao aliyechaguliwa tangu zamani. Sasa, kama hiyo Mbegu haikuwa juu ya nchi, haingeweza kuishi. Ilipaswa kuwa juu ya nchi, na pia iwe ni hai. Haidhuru itawekwa gizani kwa muda gani, itachipuka wakati M—w—a—n—a atakapoiangazia. Angalieni sasa, Yeye alikuja kushiriki Hiyo pamoja nasi.

⁶⁰ Si ajabu Injili ni habari njema. Neno lenyewe *Injili* linamaanisha “habari njema.” Habari njema, ya nini? Kama mtu fulani alikufa kwa ajili yetu, hiyo ni habari njema. Kama Kristo alizaliwa, hiyo ni habari njema. Lakini kamwe habari, kamwe hapajakuwepo na habari kama habari hii, ya kwamba, Yeye aliyefanya ahadi amekwisha thibitisha hiyo ahadi. Basi, “Yu hai milele na milele, na anazo funguo za mauti na kuzimu pia, mkononi Mwake.” Utusitusi wote uliondolewa. Hakukuweco na utusitusi tena ulioonekana, kwa maana Mwana alikuwa amefufuka kutoka kaburini. Hakukuweco na, “Vema, Yeye atakuja, ama Yeye huenda akaja.” Tayari Yeye alikuwa amekuja, Injili, habari njema!

⁶¹ Angalia, Ujumbe ule hasa wa Injili, Yenyewe, ni kuwathibitishia watu ya kwamba Yeye amefufuka. “Enendeni mkawaambie wanafunzi Wangu ya kwamba nimefufuka katika wafu, Nami nitakutana nao, kuthibitisha jambo hili kwao.” Ee Mungu, jinsi ambavyo katika hii siku ya mwisho kutakuweco na Nuru tena kote ulimwenguni! “Nami nitawathibitishia wanafunzi Wangu! Enendeni mkawaambie ya kwamba mimi si mfu, pia mimi si mapokeo, bali Mimi ni Kristo aliye hai. Nitakutana nao. Wapelekeeni wanafunzi Wangu Ujumbe huu, ya kwamba nimefufuka katika wafu,” Injili, habari njema.

Mnasema, “Hiyo ni kweli?”

⁶² Waebrania 13:8 ilisema, “Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sisi, wafadhiliwa, tunapaswa kuthibitisha Maisha Yake yako ndani yetu sasa, wafadhiliwa wa Uhai huu. Yale Maisha, hapajakuwepo na maisha yaliyoishiwa kama hayo; Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Naye alikufa, na jambo hilo likaufungia nje; bali wakati Yeye alipofufuka tena katika wafu, kwenye asubuhi ya Pasaka, ndipo sisi, kama watumishi Wake, tumeagizwa Naye kwenda ulimwenguni kote na kuileta habari hii njema kwa kila mtu, ya kwamba Yeye yu hai. Nasi tunawezaje kufanya jambo hilo kwa Neno tu? Kwa kuwa imeandikwa, “Injili haikufika kwa Neno tu, bali kwa uweza na dhihirisho la Roho Mtakatifu, kuthibitisha ya kwamba Yeye yu hai.”

⁶³ Sasa, kama kuna injili nyingine, kama alivyonena Paulo kwa moja ya yale makundi, “Ninashangaa sana ya kwamba mmegeukia injili nyingine.” Ambapo hakuna nyingine, ila injili ya kujifanya kuamini, kwa hadithi ya kimadhehebu, mkiiacha habari hiyo njema.

⁶⁴ “Na kwa sababu Mimi hi hai, ninyi nanyi mko hai. Nami ninaishi ndani yenu, na kazi nizifanyazo Mimi,” Yohana 14:12, “kazi nizifanyazo Mimi zitanitambulisha Mimi ndani yenu.” Ni Ujumbe wa namna gani! Si ajabu, tumekuwa na ulimwengu

wenye giza la theolojia, bali katika wakati wa jioni kutakuja Nuru tena. Kutakuweko na ufufuo katika wakati wa jioni. Kutakuwako Nuru wakati wa jioni.

⁶⁵ Sasa, kiini chenyewe cha Ujumbe uliotumwa, ya kwamba, “Yeye amefufuka katika wafu,” sisi wafadhiliwa Wake, sisi tunaoshiriki ule ufufuo pamoja Naye, tunapata fanaka kutoka kwenye jambo hili, kwa kuuthibitishia ulimwengu ya kwamba Yeye yu hai. Hatuwezi kutenda jambo hilo kwa neno tu. Hatuwezi kufanya jambo hilo kwa mapokeo ya mwanadamu. Tunaonyesha tu kile hasa tunachokielekezea kidole.

⁶⁶ Nahofia leo ya kwamba wengi mno wetu hawawapeleki watu kwa Kristo. Tunawapeleka kwenye kanisa, kwenye nadharia fulani. Bali hatuna budi kuwapeleka kwa Kristo. Ni Yeye pekee, na Yeye ndiye Mmoja pekee aliye na Uzima. “Yeye aliye na Mwana, yuna Uzima.”

⁶⁷ Na kama uhai wa mtu aliyekufa unaonyeshwa ndani yako, utaishi maisha yale yale aliyoishi yeye.

⁶⁸ Kama damu ya mtu fulani ilikuwa ya namna fulani, nawe ukaichukua damu hiyo kutoka kwa mtu mmoja na kuibadilisha damu ya mtu huyo mmoja kwa nyingine, yeye bila shaka kabisa angekuwa wa damu ya namna hiyo.

⁶⁹ Na kama roho yako iliyo ndani yako ikihesabiwa kwamba imekufa, nawe umetiwa upako kwa Uhai uliokuwemo katika Kristo, uko juu yako! Warumi 8:11 ilisema, “Ikiwa Roho aliyemfufua Kristo katika wafu, anakaa ndani yako, atauhuisha pia mwili wako ulio katika hali ya kufa,” uhai uo huo, nguvu zile zile, baraka zile zile, alizokuwa nazo hapa duniani, kutoka kwa Mungu. Yeye alikukomboza wewe, Mzao uliokusudiwa tangu zamani na Mungu, ambao majina yao yaliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

⁷⁰ Na hiyo Nuru ya Injili ya ufufuo, kule kuthibitishwa kwa Neno! Tulijuaje Yeye alikuwa ndiye Kristo? Kwa maana Yeye alithibitisha kile alichonena. Nitaujuaje Ujumbe wa wakati huu? Mungu huthibitisha kile alichoa hidi, Naye hunena juu yake. Hicho ndicho kitambulisho, ya kwamba sisi ni warithi pamoja Naye wa ufufuo. Yeye huthibitisha kile alichonena.

⁷¹ Yale aliyoahidi kutenda katika Kristo, Yeye ameyathibitisha kwenye ule ufufuo. Yale aliyoahidi kutenda katika siku za Musa, aliyathibitisha. Yale aliyoahidi kufanya katika siku za Henoko, Yeye aliyathibitisha. Katika siku zote za mitume, Yeye aliyathibitisha.

⁷² Sasa katika siku hii, Yeye huthibitisha aliyosema, kwa maana wao ni sehemu ya ule Mzao uliowakilishwa kwenye Kitabu cha Uzima ambacho alikuja kukikomboza akirudishe kwa Mungu tena. Loo, ni Ujumbe wa jinsi gani!

73 Kwenye ile asubuhi ya Pasaka, si kwamba tu Yeye alifufuka, bali warithi Wake walifufuka pamoja Naye. Yeye. . . Wao walikuwa ndani ya Kristo katika kusulubishwa Kwake. Walikuwa ndani Yake katika kufufuka Kwake. Sisi ni warithi Wake, waliohuishwa baada ya kufa katika giza.

74 Ulimwengu wenye giza la kutokuamini, ambapo makanisa na madhehebu, na kadhalika, yalikuwa yametuingiza. Na kuna kitu ndani yetu kinachoita, “Loo, tunamhitaji Mungu! Tunamwonea Mungu njaa na kiu.” Tulijiunga na Methodisti, Batisti, Wapentekoste, Wapresbiteri, na kadhalika, na hata hivyo kulikuweco na kasoro, hatungalilipata bado. Na mara tu, tulipokuwa tunatusatusa gizani, ule ufufuo mkuu ukatujia katika kudhihirishwa kwa Neno la Mungu lililoahidiwa.

75 Kama vile Yeye alikuwa dhahirisho la Neno la Mungu lililoahidiwa. “Sitakuachia kuzimu nafsi Yake, wala sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Yeye alidhihirisha jambo Hilo, kila Neno la Mungu aliloahidiwa. Yeye alithibitisha jambo Hilo alipofufuka kwenye asubuhi ya Pasaka.

76 Sasa, hao ambao siku moja walikuwa wakitutusa gizani na hawajui, kama wanapaswa kutawadha miguu katika siku *hii*, ama kama wanapaswa kuadhimisha siku fulani, ama kufanya kanuni fulani, mambo hayo yote yalipita. Kwa kuwa, kulikuweco na ufufuo wenye utukufu ulioasi kila kitu cha kujibunia ambacho mwanadamu aliwahi kufanya, kila sababu iliyotolewa na mwanadamu.

77 Hapakuweco na mtu, mpaka wakati huo, ambaye angeweza kuutoa uhai wake na kuutwaa tena. Yeye aliasi kanuni hiyo ya kisayansi waliyokuwa nayo, kwa kufufuka tena.

78 Wanaposema, ya kwamba, “Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele,” ya kwamba, “Uweza Wake si ule ule,” ya kwamba, “Injili Yake si ile ile,” wakati Biblia inasema ni ile ile! Mungu aliasi kila madhehebu, kila kanuni ya imani, Naye akasonga mbele na Roho Wake Mtakatifu, kama alivyoahidi, na kututhibitishia, ya kwamba Yeye yu hai.

79 Sisi ni wafadhiliwa wa kufufuka Kwake, tuliohuishwa baada ya kufa katika ulimwengu, katika dhambi na makosa. “Yeye ametuhuisha sisi pamoja Naye, akatufufua pamoja Naye, sasa tunaketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu.” Kuleta Kwake. . .

80 Roho Wake analeta Uhai Wake ule ule duniani. “Ikiwa Roho wa Mungu, aliyemfufua Kristo,” ule mwili, ule mwili uliotiwa mafuta; kama Roho wa Mungu aliutia mafuta mwili huo hivi kwamba, hiyo Mbegu ilipoanguka katika ardhi, Yeye asingalimwacha Yeye abaki humo. La. Yeye alimhuisha na kumfufua. “Roho yule yule,” kwa kazi zile zile, kwa Uweza ule ule, kwa ishara zile zile, “akiwa ndani yenu, Yeye atawafufua pia.”

⁸¹ Ningetaka kuwasomea Andiko dogo hapa. Ningewatakeni mfungue Andiko lingine nililoandika hapa. Huenda likawasaidia kidogo. Linapatikana katika Kitabu cha Mambo ya Walawi, sura ya 23, aya ya 9 hadi aya ya 11. Sikilizeni kwa makini. Katika torati, torati ya Walawi, Mungu akinena na Musa. Sikilizeni. Mambo hayo yote ni mifano sasa, nasi tutasimama hapa kwa muda mchache kuingia katika mfano huu.

*Kisha BWANA akanena na Musa, na kumwambia,
Nena na wana wa Israeli, uwaambie, Hapo
mtakapoingia hiyo nchi niwapayo, . . .*

⁸² “Kuingia mahali pale, ile sehemu, ambayo nimewapa. Sasa nena na wana wa Israeli, ya kwamba mtakapofika mahali hapa ambapo nimewaahidi nitawapeleka, mtakapofika kule kwenye nchi hii.” Sasa tukizungumza mambo ya kawaida hapa, yakiwa mfano wa ya kiroho.

*. . .na kuyavuna mavuno yake (mmepokea
niliyowaambia), ndipo mtakapomletea kuhani mganda
wa malimbuko ya mavuno yenu;*

*Naye atautikisa mganda mbele za BWANA ili
kwamba ukubaliwe kwa ajili yenu; siku ya pili baada
ya sabato kuhani atautikisa.*

⁸³ Kama kungekuwa na sherehe yo yote takatifu, ingepaswa kutokea kwenye siku ya Sabato, ambayo ilikuwa siku ya saba ya juma, ambayo ni Jumamosi. Bali mliona, katika kumbukumbu hii, utatikiswa siku ya kwanza ya juma?

⁸⁴ “Mganda, ambao ulikuwa ni malimbuko ya kwanza ya nafaka yenu mliyopanda, wakati inapochipusha na kuiva, unakata mganda huu na kumpelekea kuhani. Na kumwacha auchukue na kuitikisa mbele za Bwana, upate kibali, ya kwamba umekubalika. Umekuja na mganda wako, naye anapaswa kuitikisa mbele za Bwana, kwenye. . .”

⁸⁵ Si katika sabato, siku ya saba; bali kwenye siku ya kwanza, ambayo tunaita Jumapili, J-u-m-a-p-i-l-i.

⁸⁶ Bila shaka, hilo ni ninii—neni la Kirumi, ambayo waliita siku ya jua kwa ajili ya mungu jua. Lakini jinsi ilivyobadilika!

⁸⁷ Si j-u-a tena. Ni Siku ya M-w-a-n-a, Siku ya Mwana, ambayo hiyo chembe ya Ngano (ya Kwanza ya Mungu kutoka kwa wafu) itatikiswa juu ya kusanyiko, ya kwamba sisi ni Mzao Wake; na huyo ndiye Mzao wa kwanza wa wale waliolala mauti, akitikiswa kwenye siku ya kwanza ya juma. Jumapili, Yeye alifufuka. Akasema kwaheri, kisha akapaa Juu, mbele ya watu.

⁸⁸ Angalia, ilikuwa Punje ya kwanza ya Ngano ya Mungu ambayo ilikuwa imefufuliwa katika wafu, Punje ya kwanza ya Ngano ya Mungu. Kwa Nguvu za Mungu za Kuhuisha, Mungu

alikuwa ameuhiuisha uhai Wake, akamfufua katika wafu, Naye alikuwa Malimbuko ya wale waliolala mauti, Malimbuko. Yeye alikuwa mganda huo.

⁸⁹ Hiyo ndiyo sababu iliwapasa kuutikisa huo mganda, kwa maana ulikuwa wa kwanza kupevuka. Nao ulitikiswa kama kumbukumbu ya shukrani kwa Mungu, wakiamini ya kwamba hiyo mingine iliyobaki ingekuja. Pia ilikuwa ni ishara.

⁹⁰ Ndipo, leo, kwa maana Yeye alikuwa Mwana wa kwanza Mungu kufikia kupevuka kabisa, kuwa katika Mungu, Yeye aling'olewa kutoka ardhini na anatikiswa juu ya watu. Loo, ni somo tukufu jinsi gani! Kwa Nguvu ya Kuhuisha, Yule wa kwanza! Ingawa, alikuwa—alikuwa ameonyeshwa kwa mfano; na mara nyingi, kama tutakavyoona baadaye, ya kwamba alikuwa ameonyeshwa kwa mfano. Bali huyu kweli ni Malimbuko ya wale waliolala mauti. Yeye alitikiswa juu ya Mzao ulioahidiwa ambao ulipewa ahadi ya Uzima.

⁹¹ Yeye alitikiswa kwenye Siku ya Pentekoste, “wakati sauti ilipotoka Mbinguni kama upepo mkubwa wenye kutikisa unaoenda kasi,” naye alitikiswa juu ya watu, wapentekoste waliokuwa kule kwenye Pentekoste, wakingojea ile Baraka ije.

⁹² Naye atatikiswa tena, tunatambua, katika siku za mwisho, kulingana na Luka 17:30, katika siku ya Mwana tena, “katika siku atakayofunuliwa M-w-a-n-a wa Adamu,” ama kutikiswa tena juu ya watu.

⁹³ Sasa, Mwana wa Adamu ni nani? “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Na iwapo mafundisho yote tuliyo nayo, na thibitisho la Neno la Mungu; kwa Neno la Mungu, kwa ishara, kwa maajabu, tunaona leo, ya kwamba katika Kitabu cha—cha Luka hapa, ya kwamba kama tulivyonukuu hicho hivi punde, ama Lu—Luka sura ya 17 na aya ya 30; na Malaki 4, na Maandiko mbalimbali ambayo tunayajua, ya kwamba hilo Neno tena linatikiswa juu ya watu, ya kwamba mapokeo yaliyokufa ya mwanadamu yamekufa, na Mwana wa Mungu yu hai tena na Ubatizo wa Roho Mtakatifu moja kwa moja miongoni mwetu, naye anatupa Uzima.

⁹⁴ Kama vile Kristo alivyokuwa wa kwanza kufufuka, kutoka kwa manabii wote, na kadhalika; ingawa ameonyeshwa kwa mfano katika mahali pengi, Yeye alikuwa Malimbuko ya hao waliolala mauti. Naye Bibi—arusi, akitokana na Kristo, akitoka kanisani, itabidi kuwe na Mganda utakaotikiswa tena katika siku za mwisho. Loo, jamani!

⁹⁵ Kutikiswa kwa mganda! Mganda ulikuwa nini? Wa kwanza uliopevuka, wa kwanza uliothibitika ya kwamba ulikuwa ni ngano, ambao ulithibitika ulikuwa ni mganda.

⁹⁶ Haleluya! Nina hakika mnaona ninalozungumzia. Ulitikiswa juu ya watu. Na wakati wa kwanza utakapotokea, wakati wa Bibi-arusi, kwa ajili ya ufufuo kutoka kwenye giza la kimadhehebu, kutakuwa na Ujumbe, kwamba kukomaa kabisa kwa Neno kumerudi tena katika nguvu Zake zote, na kutikiswa juu ya watu, kwa ishara zile zile na maajabu Yeye aliyotenda kule nyuma.

⁹⁷ “Kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mu hai pia,” akinena na Mkewe. “Kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mu hai pia.” Huo ulikuwa ni ufufuo wa jinsi gani! Na huu ni ufufuo wa jinsi gani, kuhuishwa kutoka kwa wafu, “kufanywa hai katika Kristo Yesu,” na Uweza wa Mungu wa Kuhuisha.

⁹⁸ Yeye alitikiswa kwao. Neno, ambalo Yeye alikuwa, lilitikiswa tena kwao kwenye siku ya Pentekoste, Neno lililodhihirishwa. Sasa, na kama nise mavyo, litatikiswa tena katika siku za mwisho. Sasa, kwa mfano. . .

⁹⁹ Mnasema, “Vema, basi, ngoja kidogo, Ndugu Branham. Ninajua kanisa ambalo. . .” Vema, mimi ninalijua, pia. Mnaona?

¹⁰⁰ Lakini sasa, kwa mfano, vipi kama—kama tulikuwa turudi Tucson alasiri ya leo, sasa, na kila mmoja wetu alikuwa na. . . alikuwa aende na gari la Ka—Kadilaki kubwa, mpya kabisa? Na viti vyote vilikuwa vimeundwa kwa—kwa ngozi ya jike la paa, ngozi iliyo nyororo sana kuliko zote, nyororo na ya starehe kukalia; na mbao za chini zilikuwa nzuri sana; usukani ulikuwa umenakshiwa madini ya nikeli na ulikuwa na vinundu vya almasi kila mahali; na injini ilikuwa imejaribiwa kimitambo kuwa injini inayofaa kabisa; na magurudumu yalikuwa. . . yote yalikuwa na gololi na zimepakwa grisi; na tairi zote zilikuwa zisizoweza kupata pancha wala kutoka pumzi; na vyote vilikuwa vimethibitishwa kisayansi.

¹⁰¹ Yote yalikuwa yametolewa kwenye kituo cha kutengenezea magari, yote mawili, na yote mawili yamejazwa petroli. Hizo ni nguvu za kuendesha, petroli, kwa maana ina okteni. Lakini sasa utakapoanza kuyapiga stati, ingawa yote mawili yanafanana kabisa, lakini kuna moja ambalo halina spaki yo yote, nguvu zo zote za kuendesha.

¹⁰² “Vema,” unasema, “nguvu ziko katika petroli, Ndugu Branham.” Lakini sijali kuna nguvu kiasi gani katika petroli; isipokuwa kuwe na spaki mle kudhihirisha nguvu hizo, isipokuwa kuwe na nguvu fulani mle kuthibitisha ya kwamba hiyo ni petroli, afadhali hata ingalikuwa ni maji. Mpaka. . .

¹⁰³ Haidhuru wanatheolojia watadai jinsi gani, jinsi umeliweka kanisa lako vizuri, una elimu kiasi gani, jinsi ulivyo kama Biblia; mpaka huo Mganda wa kutikisa, mpaka Roho

Mtakatifu atakapokuja juu ya mtu huyo kulihuisa Neno hilo! Hiyo petroli inaliwakilisha Neno. Hilo ni Kweli; bali, bila Roho, halitatenda kazi.

¹⁰⁴ Tumeweka mkazo sana juu ya Mitambo na hakuna cho chote juu ya Nguvu za Utendaji. Inahitaji Nguvu za Mungu za Utendaji, nguvu za Ufufuo wa Yesu Kristo juu ya Kanisa, kudhihirisha na kutimiza kwamba *Hii* ni petroli. Huenda ikawa katika kopo la petroli; ingali inaweza kuwa ni maji, mnaona? Bali thibitisho pekee lake, ni, utie Uhai huu juu yake, nayo itathibitisha kama ni petroli ama la.

¹⁰⁵ Na unapojaribu kuweka Roho Mtakatifu katika madhehebu, ni kama vile unajaribu... Unaweza ukapata kutatarika; utaiharibu injini yako, kwa kuijaza kaboni.

¹⁰⁶ Lakini, lo, nina furaha sana ya kwamba kuna Nguvu za kipimo okteni cha elfu moja, Neno la Mungu na Roho Mtakatifu kuiwasha, na kuzifufua nguvu za Mungu katika maisha ya mwanamume, ama maisha ya mwanamke, ama katika kanisa. Ambayo iliisukuma ile Kadilaki barabarani kule, chini ya Nguvu za kuendesha za Roho Mtakatifu ambazo zilirudi na kutikiswa juu ya watu kwenye siku ya Pentekoste, zikimfanya yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁰⁷ Kulikuwa na Mganda wa kwanza uliojitokeza kutoka kwa manabii wote, ambao ulikuwa ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa manabii wote.

¹⁰⁸ Kumekuwako na makanisa, makanisa, mabibi-arusi, mabibi-arusi, makanisa, mabibi-arusi, mabibi-arusi.

¹⁰⁹ Bali hapana budi kuje Mmoja! Haleluya! [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.] Hakuna budi kutokee Bibi-arusi halisi! Hapana budi kutokee Mmoja ambaye hana tu Mitambo, bali Nguvu Zake za Utendaji, zinazolifanya Kanisa hilo liishi, litende kazi katika nguvu za kufufuka Kwake. Hata tutakapofikia mahali pale, hata tutakapopapata mahali hapo, ina faida gani kupiga msasa vitovu vya magurudumu? Inafaa nini kuitengeneza kwa nje ama kuisafisha na kuipaka mafuta, wakati hakuna Nguvu za Utendaji ndani yake? Haidhuru Mitambo itathibitika kuwa ni sawa jinsi gani, hapana budi kuweko na Nguvu za Utendaji kuifanya itende kazi.

¹¹⁰ Hivyo ndivyo Yeye alivyothibitisha! Haleluya! Hicho ndicho Pasaka ilichothibitisha. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Yeye hakuwa tu Neno, bali alikuwa Mungu Mwenyewe, Nguvu za Utendaji, katika Neno. Hizo zilizoufanya mwili wa Yesu Kristo (baridi, mkavu, na uliokufa, kaburini) kutikisika ukawa Hai na kufufuka tena, na kulifingirisha lile jiwe. “Mimi Ndiye niliyekuwa nimekufa,” alikufa kabisa hata jua likasema amekufa, mwezi ukasema amekufa, nyota zikasema amekufa. Maumbile yote yakasema amekufa. Na sasa ulimwengu mzima hauna budi kutambua ya

kwamba Yeye yu hai tena. Yeye hakuwa ile Mitambo tu, Neno la Mungu, Yeye alikuwa zile Nguvu za Kuendesha kuthibitisha jambo Hilo.

¹¹¹ Na kwa kuwa Yeye, akiwa Bwana Arusi, Bibi-arusi hana budi kutokea, kwa maana Yeye ni sehemu Yake. Na inaweza tu kuwa ni kudhihirishwa kwa kutimizwa kwa funuo zingine zo zote zilionena juu ya Bibi-arusi; inaweza tu kudhihirisha. Kama akifanya kitu tofauti na Bwana Arusi, si Bibi-arusi. Kwa maana, Yeye ni nyama ya nyama Yake, mfupa wa mfupa Wake; Uhai wa Uhai Wake, nguvu za Nguvu Zake! Yeye ni Yeye! Kama vile mwanamume na mwanamke ni mmoja, na mwanamke alitolewa ubavuni mwake; Yeye amechukua Roho Wake, Roho ya kike, kutoka Kwake. Nyama kutoka ubavuni Mwake, akafanywa Mitambo na Nguvu za Utendaji pia, huyo Mke. Roho Yake na mwili Wake, akaviweka pamoja, kisha akafanya Mitambo pamoja na Nguvu za Utendaji. Mpaka kanisa ama watu . . .

¹¹² Hii mikate midogo yote ya Pasaka, na sherehe, na makanisa makubwa, na umalidadi, vitashindwa na kupita.

¹¹³ Mpaka Kanisa hilo litakapokuwa Mitambo na Nguvu za Utendaji pia; na Roho wa Mungu, aliyemwongoza Yeye, kufanya mambo aliyoyafanya! Kama alikumbana na yenye silinda kumi na sita, vivyo hivyo Bibi-arusi naye. Amina! Kwa kuwa alisema, katika Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Nitamtia chaji ya Nguvu Zangu za Utendaji, katika Mitambo yake, ambayo ulimwengu hautaweza kuistahimili; nami nitamfufua tena katika siku ya mwisho!” Huo ndio Ujumbe wa Pasaka, Nguvu za Utendaji na Mitambo, pamoja! Mitambo bila ya Nguvu za Utendaji, haifai kitu; wala Nguvu za Utendaji, bila Mitambo.

¹¹⁴ Unaweza kupiga makelele na kupaza sauti, na kurukaruka, utakavyo, na kulikana Neno hili, haitakufaa kitu. Unazungusha tu mpini kwenye pi—pistoni za . . . Una spaki ya kuiwasha, bali hakuna petroli ya kuiwasha.

¹¹⁵ Hizo zitafanya kazi tu zinapokutana. Amina! Kwa hiyo, mmoja ataketi kimya, na huyo mwingine atanyakuliwa. Hakuna lingine. Hata hivyo, wote wawili wanaweza kuonekana sawa, wote wawili wanadai kuwa ni makanisa, wote wawili wanadai kuwa ni Bibi-arusi. Bali mmoja ana Mitambo na Nguvu za Utendaji, Hizo zinatimiliza, yale aliyosema ni Kweli.

¹¹⁶ Haitatenda kazi kamwe, hata Mitambo iwe mizuri jinsi gani, hata Nguvu za Utendaji zitakapokuja. Nguvu hizo za Utendaji zitakapokuja, huo Moto unafanywa kushikana na okteni hiyo iliyo kwenye petroli. Basi wakati hiyo inapolipuka, inaanzisha mwako, na mwako huo unasogeza kila mwendo, kila hatua, kwa maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Huo ndio ufufuo. Hizo ndizo Nguvu halisi za Mungu, Mitambo pamoja na Nguvu za Utendaji. Angalia, “Roho ndiye anayehuisa.” Ndiye ile—ile spaki inayowasha moto. Petroli siyo inayowasha moto; Spaki ndiyo inayoiwasha petroli. Mnaona?

¹¹⁷ “Hamwezi kufanya lo lote bila Mimi; bali mkiwa pamoja Nami mnaweza kufanya mambo yote.” Kwa kuwa Yeye ni Neno; ni Baba anayeishi. “Baba alivyunituma Mimi, Mimi Nami nawapeleka ninyi. Kama vile Baba alivyoniwasha Mimi moto na kunisukuma akaniingiza kwenye kila kitu, Mimi hufanya tu yale yanayompendeza Mungu. Naam, kama vile Yeye alivyunituma, vivyo hivyo nawapeleka pamoja na Mitambo ii hii, na inahitaji Nguvu zile zile za Utendaji kuiendesha. Na ishara hizi zitafuatana na hao wanaodai kuwa na Mitambo. Nguvu za Utendaji zitapachukua mahali pake.”

¹¹⁸ Paulo alisema, “Injili ilitufikia si kwa Neno tu,” kwa petroli tu, bali kwa Spaki pia,” kulifanya Hilo litende kazi. Hivyo ndivyo ilivyo. Ilitufikia kwa njia hiyo.

¹¹⁹ Ni Roho yule yule, aliyemfufua Yeye, ndiye aliyemhuisa muumini wa kweli kupata Uzima wa Milele. Sasa kumbuka, kwa uwezekano. . . Sasa angalia, kwa kuwa tunaishiwa na wakati. Angalia, “Roho yule yule,” sasa, Warumi 8:1. Sasa hebu na tusome tu hilo tena, katika Warumi 8:1, nasi tutaona yale hilo linasema. Vema. Na si Warumi. . . Namaanisha, 8:11, samahani.

¹²⁰ Katika Warumi 8:11, “*Lakini ikiwa. . .*” Hapo ndipo penye shida. Mfumbato Wake ndio huo.

Lakini, ikiwa Roho wake yeye (Mungu, Roho Mtakatifu) aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, . . .

¹²¹ Sasa, haya basi, “Ikiwa Roho ya Bwana Arusi anakaa ndani ya Bibi-Arusi!”

¹²² Wakati Mungu alipomfanya bwana-arusi Wake wa kwanza, yeye alimfanya bwana arusi kwanza, naye alikuwa mwanamume na mwanamke pia, katika roho; akamfanya katika mavumbi ya ardhi, kumfanya awe mwili wa nyama na damu. Na angalia wakati Yeye alipomfanya Hawa, kutoka kwa Adamu, Yeye hakutwaa kipande kingine cha udongo, alitwaa kutoka kwenye kipande kile kile cha udongo; Neno lile lile, kwa kuwa Adamu alikuwa Neno lililonenwa. Mnaona? Yeye alitoa kwake, halafu akachukua ile. . . Yeye alikuwa na roho ya kiume na ya kike. Naye akaitoa roho ya kike kutoka kwa Adamu, na kuiweka katika Hawa; kwa hiyo ingali ni sehemu ya roho ya Adamu, ni mwili wa Adamu. Basi, ilikuwa ni roho ya Adamu, zile nguvu za utendaji, ambazo ziliihuisha mitambo ya mwili wake.

123 Vivyo hivyo Bibi-arusi hana budi kuwa pia nyama ya nyama Yake, na mfupa wa mfupa Wake. Basi mwili huu unaopatikana na mauti utafanyikaje mwili Wake? Tutalifikia hivi punde, mnaona. Inatendekaje? Vipi? Badiliko hili kuu ni nini? Angalia.

Basi ikiwa Roho wake yeye (Mungu) aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.

124 Loo, jamani! Waliochaguliwa tangu zamani, bila shaka, kama Mbegu iliyokuwa ardhini, Hao waliokuwa na Uhai ndani yao. Wengi wao walikuwa wamekufa; wao walikuwa tu mbegu zilizoza; maji na kadhalika viliwachoma. Bali, unajua, kulikuwako na Mbegu iliyokaa kule ikiwa tayari kwa ajili ya Uzima. Mungu alijua ilikuwa imekaa pale.

125 Sasa, Hao waliochaguliwa tangu zamani ndio wa kwanza kuhiuisha na Roho Mtakatifu, kwa kuwa Roho Mtakatifu huja kuwadau Walio Wake. Sasa, hili lina kilindi sasa, na hakikisheni mtalishika vizuri.

126 Sasa, kama vile jua lilivyotumwa kote duniani, si kusababisha miamba, ambayo ilikuwa taka pia, iwe hai, halikuwa lifanye takataka zote hai, bali ilikuwa ilete ile sehemu ya takataka iliyokuwa imefunika uhai fulani.

127 Si watu wote watakaompokea Kristo. Loo, la. Bali wale Mungu aliowakusudia Uzima tangu zamani, wamefunikwa na takataka zingine za dunia, hao ndio Yeye anaokuja kuwahuisha. Ni hao.

128 Hiyo, sasa, huo udongo ungekaa pale juani, na kusema, "Loo, jua hili la kale ni kali sana!" Huo mwamba, useme, "Jua hili la kale ni kali sana!" Bali ile mbegu ndogo, ilisema, "Hilo ndilo ninalotafuta," nayo inaanza kuchipuka iwe hai. Lilihuisha sehemu huo ya udongo. Kwa kuwa, jua lilitumwa si kuuhuisha mwamba, si kuuhuisha udongo, bali kuuhuisha uhai wa ile mbegu.

129 Sasa, Roho Mtakatifu huja sasa. Bila shaka, hakutumwa . . . Kwa nini watu wote hawatampokea? Yeye hakutumwa kwao.

130 Jamaa fulani aliniambia, "Siamini. Sijali ungesema nini. Kama ungaliweza kuwafufua wafu, ama cho chote kile, na kuwaponya wagonjwa; na kuthibitisha jambo Hilo, kwa njia yo yote; bado siamini jambo Hilo."

131 Nikasema, "La hashu. Wewe ni asiyeamini. Halimaanishi cho chote kwako. Hilo hata halikutumwa kwako. Lilitumwa kwa wale watakaoamini."

132 Ujumbe ni kwa muumini. Kwao wanaoangamia, ni upumbavu; bali kwa wale walio katika Kristo, na ni sehemu ya Mzao yule, ni Uzima.”

133 Hadithi yangu isiyo nzuri sana juu ya yule mkulima aliyeweka yai chini, ama yai la tai chini ya kuku. Mnaona? Tai huyo mdogo alikuwa, kabisa, yeye alikuwa—alikuwa akionekana maskini kiumbe cha kipekee. Wakati mkulima huyu alipokwisha kufanya jambo hilo alilofanya, kuweka yai hili la tai chini ya maskini kuku huyu. Naye akaangua kifaranga aliyeonekana wa kuchekesha, naye alikuwa—alikuwa maskini jamaa mdogo wa kipekee. Hakufanana nao, manyoya yake hayakuwa kama ya hao wengine, naye—naye alikuwa tu...Alikuwa jamaa mdogo wa kipekee. Na hao vifaranga wengine wote wakamtambua kama jamaa wa kipekee. Naye yule kuku akaenda huku na huko...

134 Yeye hata hakupendezwa na mlo aliokuwa anampa. Kwa kweli hakupenda kule kukwaruza—kwaruza kwenye kitalu. Yeye, hakuhusika na jambo hilo. Kwa hiyo hakujuu ni kwa nini alilazimika kuwa wa kipekee hapo, hata hivyo. Mnaona? Naye hakupata kuonja kitu cho chote ambacho...Alikula tu cha kutosha kumfanya aishi, kwa maana hakuipenda ladha yake, mnaona. Kwa maana, yeye hakuwa kuku, kwanza. Mnaona?

135 Naye hu—huyo kuku angelia, na, mwajua, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho. Jiunge na kanisa.” Hilo halikuonekana sawa, kwa jamaa huyo mdogo. Kwa hiyo yeye alifuatana na huyo kuku mpaka siku moja mamaye...

136 Maskini yule tai alijua alikuwa ametaga kiasi fulani cha mayai, na kulikuwa na moja lililokosekana. Alijua ya kwamba tai huyo alikuwa mahali fulani, kwa hiyo akaanza kwenda kumtafuta. Ndipo akazunguka juu ya milima, na chini mabondeni, na juu ya kila mahali ambapo angeweza kuwa. Kufikia wakati huu, yeye, ni wakati wake wa kuzaliwa. Ni wakati wake wa kuanguliwa. Kasema, “Labda kunguru alikuja akalichukua yai langu; labda koho. Sijui. Kitu fulani kililichukua yai langu. Bali najua...Yai hilo liko moyoni mwangu. Nina mwana mahali fulani. Sina budi kumtafuta.”

137 Ndivyo afanyavyo Mungu. Yeye ndiye yule Tai Mkuu. Katika mawazo Yake alijua angekuwa na Kanisa fulani. Yeye alijua angekuwa na watu fulani. Haidhuru ni nini kimewakumbatia, haidhuru wameanguliwa chini ya nini, Yeye anawatafuta. Anawatafuta Walio Wake.

138 Na siku moja, hiyo hadithi inasema, maskini huyu tai aliruka kupitia juu ya kile kitalu. Alikuwa akitafuta kila mahali, ndipo akampata. Loo, kwa ajili ya ule ufufuo, kutambua ya kwamba yeye hakuwa kweli kuku, hata hivyo. Alikuwa tai! Naye daima alifundishwa kuangalia chini,

kutafuta mdudu ama kitu fulani kwenye kile kitalu. Bali akasikia mlio, uliosema, “Inua kichwa chako uangalie *huku!*” Ndipo akaangalia juu yake, na kulikuwa na kiumbe mwenye mabawa ya futi kumi na nne, mwenye nguvu zaidi kuliko kuku wote waliokuwemo kwenye kile kitalu, naye alidai kwamba ni mwanawe.

Akasema, “Mama, nitawezaje kukufikia ?”

¹³⁹ Kasema, “Ruka tu, anza kupigapiga mabawa yako, kwa maana wewe ni tai.”

¹⁴⁰ Mnaona, Yeye alijua alikuwa na mwana mahali fulani. Haidhuru alilelewa wapi, yeye ana mwana mahali fulani.

¹⁴¹ Naye Mungu anajua! [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Haleluya! Yeye ana Kanisa lililochaguliwa na kukusudiwa tangu zamani! Yeye alijua ana wana na binti, na Bibi-arusi, anayengoja mahali fulani; wakati Roho Mtakatifu anapoanza kuruka juu yake, Mganda huo wa kutikiswa. Loo, jamani! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Si hadithi fulani ya kubuniwa, bali ni halisi!

¹⁴² Haidhuru ni wangapi waliojaribu kumwambia, “tai,” yeye hakujua tai alikuwa nini. Hata hivyo, yeye alikuwa tai. Yeye asingefahamu jambo hilo mpaka alipoona kitu ambacho kilifanana naye, ambacho alifanana nacho, hasa.

¹⁴³ Na wakati ambapo tunaona, si madhehebu, si Ph.D, si LL.D, si jirani mwema; bali mwana wa Mungu aliyefinyangwa katika sura ya Mungu, kwa Nguvu za kutenda kazi za Mungu kujibu ombi la siku hii, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hakuna kuku atakayekushikilia. Yeye humtafuta mamaye. Yeye ni tai, kwanza. Anatambua. Tai huyu halisi hutambua wito wa Neno la Mungu. Kwa nini? Yeye ni tai. Tai kwa tai! Neno kabla ya kuwekwa misingi, Neno kwa Neno! Neno, lililochaguliwa tangu zamani, kwa Neno lililoandikwa kwa ajili ya saa hii. Unatambua mahali pako. Yeye hupatafuta.

¹⁴⁴ Huu basi, mwili huu ulio wa dunia hii, unahuishwa na kuletwa na Roho wa Mungu ahuishaye upate kulitii Neno la Mungu.

¹⁴⁵ Upesi. Wakati alipotaka kujua jinsi angaliweza kufika kule awe pamoja naye, Yeye alikuwa amefundishwa asingeweza kufanya jambo hilo. “Huwezi kupaa juu zaidi ya unavyoweza kuruka.” Yeye ni kuku. Mnaona?

Bali tai huyu akasema, “Sivyo.”

“Vema, waangalie hawa kuku!”

¹⁴⁶ “Haidhuru hao kuku ni nini, wewe ni tai. Anza tu kuyatandaza mabawa hayo, na ufanye mazoezi madogo nayo. Anza kuruka juu!”

¹⁴⁷ Neno kwa Neno! “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye

naye atazifanya.” Mnaona? “Kwa sababu Mimi ni hai, yeye naye ni hai.” “Basi ikiwa Roho aliyemfufua Yeye katika wafu anakaa ndani yenu, Yeye anaihuisha miili yenu iliyo katika hali ya kufa.” Mnaona?

148 Inafanya nini? Sasa sikilizeni, ili kwamba mpate kujua. Na Pasaka hii, nataka iwe na maana zaidi kwenu kuliko Pasaka yo yote ilivyowahi kuwa. Mnaona? Nawatakeni mwone jambo hilo. Tunajua ilivyomtendea Yeye; bali nawatakeni mwone, si ati itafanya, tayari imeishafanya jambo lile lile kwa ajili yenu. Mnaona? Inafanya nini? Inauhuisha mwili ulio katika hali ya kufa. Mwili huu ulio katika hali ya kufa tunaoishi ndani yake, Hiyo inauhuisha, kwa maneno mengine, inaufanya uwe Hai.

149 Sasa, ninyi ambao wakati mmoja mlitembea mkiwa na msokoto mkubwa mno midomoni mwenu, na kila kitu, ama lundo la sigara; nanyi wanawake ambao wakati mmoja mlikuwa na nywele fupi, mkajipodoa, na kufanya yasiyofaa, na kuvaa kaptura, na vitu kama hivyo; mara moja, Kitu fulani kilipiga makelele, nawe ukatazama hapa chini na Hicho kilikuwa ni Neno. Mnaona, lilihuisha ninii yenu. . . Ulisema, “Sitaki kaptura tena, sitaki pombe tena, sitadanganya tena, sitaiba tena, sitafanya *hili, lile*.” Mnaona? Roho aliyemfufua katika wafu, akikaa ndani yenu, pia ataihuisha miili yenu iliyo katika hali ya kufa, mavumbi ya nchi, kutiishwa. Mnaona? Ni nini? Kutiishwa chini ya nini? Kristo. Kristo ni nani? Lile Neno. Si theolojia, bali lile Neno!

150 Halafu mnasema, ya kwamba, “Mambo haya, loo, nafikiri ni sawa kwa wanawake kuvalia suruali ndefu.”

151 Ambapo, Neno lilisema, “La.” Mnaona, linakuhuisha kwa jambo Hilo. Mnaona? Unavutwa Nalo. Mnaona, ni wewe, basi. Linakuwa. . . Unakuwa sehemu ya Neno. Iliuleta mwili wako, si. . .

152 Vema, unasema, “Vema, sasa, hebu nikwambie jambo fulani. Mchungaji wangu. . .” Sijali alichosema mchungaji wako; ni kile lisemacho Neno! Kama unataka kuwa kuku, ambatana nao. Bali kama mchungaji akinena mengine mbali na Neno hili, basi yeye si mlishi wa tai; a-ha, yeye ni mlishi wa kuku, mnaona, si wa tai. Mnaona? Tai hula Chakula cha tai. Mnaona? Linahuisha!

153 Biblia ilisema ni vibaya kufanya jambo hilo, basi mtu huyo na kadhalika na yote ninyi nyote mfanyayo, ni makosa. Asema, “Siku za miujiza zimepita.” Biblia hii ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama wao wakisema, “Huo ni uwezo wa kushirikiana mawazo. Na ni namna fulani ya kuyasoma mawazo, utambuzi huu. Na maono haya yote na kadhalika, ni upuuzi,” mnaona, wao ni kuku. Hawajui Chakula cha tai ni nini.

¹⁵⁴ Lakini, ndugu, unaposikia mlio huo, kuna Kitu ndani yako! Wewe ni tai, kwanza. Kwa nini? Wewe ni ule Mzao, ambao kule kufufuka kwa M-w-a-n-a kumekuzukia, na ule Mganda wa kutikisa juu ya nchi, kukufanya utambue ya kwamba wewe ni tai wala si kuku wa kimadhehebu. Mnaona?

¹⁵⁵ “Naam, ikiwa yule Roho aliyemfufua Yeye katika wafu,” Neno, Nguvu za Utendaji za Neno, “anakaa ndani yako, Yeye pia huuhuisha mwili wako ulio katika hali ya kufa.” Sasa sisi ni mwili wa mwili Wake na mfupa wa mfupa Wake namna gani? Kwa sababu, upesi, tulipokuwa tungali wenye dhambi walio katika hali ya kufa, wapatikanao na mauti, tayari kufa, miili hii, Hiyo inauhuisha mwili huo. *Kuhuisha* ni nini? “Kufanya Hai.” Roho ambayo wakati mmoja ilipenda kunywa pombe, kurandaranda, kufanya uzinzi, na haya yote, imehuishwa; mbona, kitu hicho kilikufa, nawe umefufuliwa. Inauhuisha mwili wako ulio katika hali ya kufa.

¹⁵⁶ Kwa hiyo, mwili wako ni hekalu la Nguvu za Utendaji. Kwa sababu (gani?) tangu mwanzo wewe ni sehemu ya ile Mitambo. Loo! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Huo hapo ufufuo wako. Hilo hapo Kanisa katika ufufuo, pamoja Naye. Miili hii hivi sasa imehuishwa. Mnaona, mmesikia; mnaamini. Ilikubadilisha kutoka kwenye madhehebu ukaingia katika Neno. Unaona?

¹⁵⁷ Nguvu za Utendaji, kama Hizo zikishukia maji, yatatarika tu; “Siku za miujiza zimepita.” Pup—pup—pup, “Loo, ninaamini Biblia,” pu-pu-pu, “lakini hakuna—hakuna. . .” Pu-pu-pu! Mnaona?

¹⁵⁸ Bali anapoangukia hicho kipimo cha okteni elfu moja, “Yuuuuu,” linaenda zake, mnaona. Vipi, jamani, zile Nguvu za Utendaji zinaangukia Hicho! Bali kama zikimwangukia kuku, hazitamfaidia kitu. Bali zinapomshukia tai, yeye hutoka anaenda. Amina! Nguvu za Utendaji pamoja na Mitambo! Mnaona ninalomaanisha? Hiyo ni kusema, endapo yeye ni tai wa kweli sasa, “atafahamu.”

¹⁵⁹ Hebu nifafanue Andiko fulani dogo hapa kwa ajili yenu. Nafikiri simu imekatwa, bali tungali tupo hapa. Yohana Mtatakatifu. 5:24, Yesu alisema, “Yeye alisikiaye Neno langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele.” Sasa angalia, nashuka naenda mtaani na kuchukua hilo lisemavyo, jinsi lilivyo, bila ufahamu wa kiroho. . .Bila kulifanya liseme jambo lingine lo lote, bali kusema tu yale linayosema, mnaona, neno linalofaa pale, katika Kiyunani, katika kile cha asili, linasema, “Yeye aelewaye Neno Langu.”

¹⁶⁰ Sasa, kuthibitisha hilo ni kweli. Nashuka kwenda hapa, na hapa yuaja mlevi barabarani, huku amemkumbatia mke wa mtu mwingine, anatumkana, na kuapa bure kwa Jina la Mungu,

na kadhalika namna hiyo. “Aisee, ulisikia yale yule mhubiri aliyosema? Ulisikia?” “Naam, nilisikia!” Hilo halimaanishi ana Uzima wa Milele. Mnaona? Mnaona?

“Yeye aelewaye Neno Langu,” yeye aliye tai!

161 “Naam, Ndugu Branham, nataka Maandiko mengine zaidi.”

162 Vema, “Kondoo Zangu huisikia Sauti Yangu. Mgeni hawatamfuata.”

163 Kama vile katika kile kisa cha *Ndoa Na Talaka*, juzijuzi. Wakati Roho Mtakatifu alipokuwa ameniambia jambo hilo, nilikuja nikalisema jinsi vile tu Yeye alivyoniambia.

164 Bibi fulani mhudumu akanikemea kwa ukali sana kidogo kwa kupiga makelele. Akasema, “Nadhani unapachukua mahali pa Mungu?”

Nikasema, “La, mama.”

165 Kasema, “Vema, uliwaambia dhambi zao zimesamehewa.” Kasema, “Wapi?,” kasema, “Mungu tu Ndiye aliye na uweza.” Mnaona, Mfarisayo mwingine. Mnaona? . . . ? . . .

166 Nikasema, “Unaona, ili kwamba upate kujua, ya kwamba, Yesu alimwambia Petro na wale mitume, baada ya yeye kuwa na ufunuo kwamba Yeye alikuwa ni Nani.”

Akamwambia, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu.”

167 Yeye alisema, “Heri wewe,” mnaona, “Bar-Yona; mwili na damu havikukufunulia hili kamwe, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amelifunua Hilo. Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; milango ya kuzimu haiwezi kulishinda. Nami nakupa wewe funguo; lo lote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni; lo lote utakalofunga duniani. . . .”

168 Huo ni ule ufunuo wa Kiungu wa Neno lililofanyika mwili. Kama lilikuwa mwili katika siku hiyo kwa njia ya Mwana, Bwana Arusi, ni mwili leo kwa Bibi-arusi. Mnaona? “Wao wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; wo wote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa.”

169 Sasa, kanisa Katoliki walichukua hilo na kulipeleka kwa makasisi wao, hilo ni kimwili.

170 Angalia, Neno la kiroho lililofunuliwa ndilo lililofanya jambo hilo!

171 Hiyo ndiyo sababu aliwaambia waende wakabatize katika “Jina” la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Alijua wao walijua Yeye alikuwa ni Nani.

172 Nikizungumza na maskini mhubiri mmoja juzijuzi, yeye aliniambia, akasema, “Sasa, Ndugu Branham, nimetoka na kujiunga, nikaenda kwenye kanisa *fulani*, kanisa la Kipentekoste.”

173 Ambapo, Wapentekoste sasa wameanza kula mkate mdogo mwembamba wa mviringo, mwajua. Mmesikia jambo hilo, nafikiri; ile kosha, mungu mwezi, mwajua. Nao wote waliikubali na wanaila. Mtu huyu alisema... Ku—kusanyiko lake lilimwendea; akasema, “Ninachobariki kimebarikiwa.” Naam, hivi hilo si ndilo kasisi husema; ana “uwezo kuugeza ukawa mwili wa Kristo”? Mnaona, ni sita ya kitu kimoja na nusu dazani ya kingine, ni jambo lile lile tu.

174 Naye akasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani.” Alikuwa anajaribu kuepa swali la Ubatizo katika Jina la Yesu, kwa sababu huyu ndiye mtu yule aliyesema m—mpinga Kristo ndiye aliyefanya jambo hilo. Akasema, “Unafikiri ni sharti mtu abatizwe katika Jina la Yesu Kristo?”

Nikasema, “Ndiyo, bwana!”

175 Akasema, “Baada ya yeye kubatizwa katika jina la ‘Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?’”

176 Nikasema, “Ndio, bwana. Yeye hajabatizwa, hata kidogo. Mnaona? Hajabatizwa, hata kidogo; hamna Jina. Hicho ni cheo.” Nikasema, “Hautambuliwi.” Nikasema, “Mbona—mbona Petro aliniii...”

177 Akasema, “Vema, sasa, hebu nikwambie jambo fulani.” Akasema, “Sasa, katika Matendo 10:49, alisema, ‘Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia.’”

178 “Lakini,” nikasema, “aligeuka moja kwa moja akasema, ‘mtu anaweza kukataza maji hawa wasibatizwe?’”

179 Akasema, “Vema, ulikuwa ukizungumza pale, muda kidogo uliopita, juu ya Matendo 19, ambapo Paulo alipita kati ya nchi za juu za Efeso, akawapata hao wanafunzi.” Kisha akasema, “Mbona,” kasema, wao hawakuwa wamebatizwa katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.”

180 Nikasema, “La, walikuwa wamebatizwa ‘kwa ajili ya toba,’ si kwa ondoleo la dhambi. ‘Kwa ajili ya toba,’ kwa maana Yesu hakuwa amejulishwa bado. Ile Dhabihu ilikuwa bado kuuawa.”

Akasema, “Vema, kwa nini iliwabidi kubatizwa tena?”

181 Nikasema, “Yule mtu aliyekuwa na zile funguo, alisema jambo hili, ‘Na ijulikane kwenu ya kwamba hapana jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu, litupasalo sisi kuokolewa kwalo.’”

182 Wokovu pekee unatolewa katika Jina la Yesu Kristo. “Lo lote ufanyalo kwa neno au kwa tendo, yafanye yote katika Jina la Yesu Kristo.” Hakuna jina jingine, hapana kanisa, hakuna ukasisi, hakuna vyeo, wala cho chote kile! Hata hivyo, Yeye ni Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Mabondeni, Nyota ya Asubuhi, Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho, Yehova-yire, -rafa, -

manasse, yote haya. Yeye ni mambo haya yote, bali hata hivyo Yeye. . . Hakuna wokovu kamwe katika cho chote cha vyeo hivyo; *Yehova*, hapana wokovu; *Ua la Uwandani*, ingawa ndivyo alivyo Yeye, hapana wokovu; *Baba, Mwana*, ama *Roho Mtakatifu*, hapana wokovu. Ni Jina la “Yesu Kristo tu!” Halafu Biblia ilisema, ya kwamba, “Habari ya toba na ondoleo la dhambi havina budi kufundishwa katika Jina Lake, kuanzia Yerusalemu, na hata pande za mwisho za nchi.”

Akasema, “Unafikiri inaleta tofauti yo yote?”

183 Nikasema, “Bwana, nataka kukuuliza jambo fulani.” Mimi na Yeye, na mke wangu, tulikuwa tumeketi mezani. Alikuwa amehamia hivi karibuni, . . .? . . . Nikasema, “Sisi sote ni Waarizona; tunaishi hapa. Nami, nasi tunajua halmashauri yetu, na wadi yetu, na kadhalika, na meya wetu, gavana, kila kitu.”

Akasema, “Naam.”

184 Nikasema, “Basi, kama nilikwambia, ndugu, wewe, ‘Uende huku ukaandikishe chakula chetu cha jioni, katika Jina la Gavana wa Mkoa wa Arizona,’ ungeenda kutia sahihi namna hiyo? Je! unafikiri wangepokea mezani?”

185 “Mbona,” akasema, “nafikiri haiwezekani.” Akasema, “Kwa nini Yesu alisema jambo hilo?”

186 Nikasema, “Jambo ndilo hili, mnaona. Kwa nini? Kama nilikwambia ‘uende ukaandikishe chakula hiki cha jioni, katika jina la Gavana wa Mkoa wa Arizona,’ nasi tukiwa wenyeji wa Arizona, nasi tunamjua huyo Gavana ni nani, mbona, ungejua kukiandikisha katika jina la ‘Sam Goddard,’ unaona.” Nikasema, “Kwa sababu, yeye ndiye Gavana wa Mkoa. Sina haja ya kukuuliza swali. Unajua huyo Gavana ni nani. Basi, wakati Yeye aliposema, ‘Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,’ Yeye alijua jinsi watakavyobatiza. Walijua Yeye alikuwa ni Nani! ‘Kondoo Wangu wanaisikia Sauti Yangu.’ Mnaona? Mnaona?”

Akasema, “Loo, kumbe.”

187 “Lakini sasa, jambo linalofuatia ni, je! utaamini? Mnaona? ‘Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele.’ Na huu Uzima mpya wa Milele unapokaa ndani yenu, Huo ndio ule uwezekano.

188 Wakati umempokea Roho Mtakatifu huyu sasa, waliyempokea katika Pentekoste; wao walikuwa ni mitambo, sasa Nguvu za Utendaji zilipaswa zije. Walikuwa wameamini. Mnajua, marafiki wetu wazuri wa Kibatisti hutuambia, “Tunapoamini, tumempokea Huyo.” Bali, wao hawakuwa Naye, ingawa walikuwa wameamini.

189 Matendo 19, wao walikuwa wameamini, bali hawakuwa Naye. “Je! mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Mnaona? Wao walikuwa na Mitambo, kweli, kwa maana mitume walikuwa...Ama, namaanisha, Apolo alikuwa anawafundisha na kuthibitisha kwa Biblia, ile Mitambo, ya kwamba Yesu alikuwa Kristo, bali wao hawakuwa na zile Nguvu za Utendaji bado. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Vema.

¹⁹⁰ [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]...-tambo, kwa uwezekano una ile bayana, kule kungoja.

¹⁹¹ Sasa, unapopata zile Nguvu za Utendaji, umehuishwa kutoka anayepatikana na mauti ukawa asiyeptikana na mauti. Inaufanya mwili wote ulitii Neno. Litakufanya utende tofauti, uonekane tofauti, uishi tofauti. Hilo litakufanya tofauti tu.

¹⁹² Sasa angalia. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]... umehuishwa. “Ninyi mliokuwa mmekufa katika dhambi na makosa, na giza, Yeye amewahuisa.” Kwa kitu gani? “Roho Wake aliyemfufua Yesu,” asubuhi ya Pasaka, “katika wafu. Na kama anaishi ndani ya miili yenu iliyo katika hali ya kufa,” sasa angalia, “Pia inahuisa, inafanya Hai, inautiisha kwa Neno.”

¹⁹³ Sasa, wawezae kudai ya kwamba una huyo Roho, halafu ujitupe mbali na Neno? Umehuishwa na kitu kingine. Kwa kuwa, Huyo ataihuisha kwenye Neno miili yenu iliyo katika hali ya kufa. Hakika, ataihuisha.

¹⁹⁴ Huwezi kutenda kazi bila Yeye. Utatatarika tu, kama huamini Hilo lote. Kama sehemu yako moja ni petroli na sehemu nyingine ni maji, huendi po pote. Unaona? Huna budi kuichukua ikiwa asilimia mia moja, petroli. Usipofanya hivyo, unaalika, wala huna nguvu. Unaona? “Bali mimi ni—ninaamini jambo *hili*, bali siamini jambo *Lile*.” Pup-pup-pup-pup. Huendi po pote.

¹⁹⁵ Lakini, loo, unapochukua utimilifu! Hebu ishike moto kwa jambo hilo, kila Neno ni Kweli.

¹⁹⁶ Halafu angalia sasa, tunapofunga, angalia jambo hili. Angalia, ni kama tu mbe—mbegu ndogo iliyo ardhini.

¹⁹⁷ Sasa, kwa uwezekano, umefufuka. Umefufuka unapompokea Roho Mtakatifu ndani yako. Umefufuka papo hapo. Mwili wako kwa uwezekano umefufuka.

¹⁹⁸ Angalia mbegu ndogo. Hebu ipande ardhini. Haina budi kunywa kutoka kwenye chemchemi Yake, maji yanayomwagika chini. Na inapoyanywa, inajisukuma juu kumwelekea Yeye, ikizidi kufanana na ile mbegu iliyoingia ardhini. Mnaona?

¹⁹⁹ Kanisa limekuja namna hiyo, kupitia kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, sasa linachanua. Mnaona? Roho wa Mungu alipitia njia hiyo.

²⁰⁰ Na roho ya ulimwengu imekuja kupita kwa mpinga Kristo, namna ile ile, na sasa inachanua katika muungano mkuu wa makanisa, mnaona, kitu chote kizima.

²⁰¹ Na mtu binafsi huja jinsi hiyo. Kila kitu hutenda kazi vivyo hivyo, katika kipimo kile kile cha Mungu, maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Angalia, njiani, unapoendelea kukua kufikia ukamilifu wa ufufuo, ukiongozwa na Roho!

²⁰² Kama vile jua, j-u-a, linavyovuta huo mmea mdogo unaokunywa kutoka kwenye chemchemi ya Mungu, unaendelea tu. . . Mnaona, unaweza tu kunywa kutoka kwenye kitu kimoja. Hebu umwage mafuta juu ya mbegu hiyo ndogo wakati mmoja; utaiua. Hiyo ni kweli. Ukimwaga maji yaliyooza, maji ya siku nyingi yasiyofaa kitu, yameharibika, yatadumaza kukua. Haitazaa matunda. Hiyo ni kweli? Lakini hebu mwagia maji mazuri na matamu kweli ya mvua, amina, hayana kemikali za kujitengenezea ndani yake, acha yatoke tu kutoka anga za juu, kisha uangalie huo mmea mdogo. Hakuna maji yatakayokuza huo kama maji hayo ya mvua. Ukiweka klorini na kadhalika ndani yake, kama vile unavyojaribu kutunyweshwa sisi nayo, na, muda si muda, inaua tu mmea huo.

²⁰³ Hiyo ndiyo shida leo. Wao wanajaribu kuwapa maji kutoka kwenye kisima cha kimadhehebu, nayo yanadumaza kukua. Mnaona? Bali hebu yeye awe na. . .

Njoo ambapo matone ya umande wa neema
yanang'aa;
Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Ndipo umelipata, basi.

Tutatembea Nuruni, ile Nuru nzuri,
Huja kutoka ambapo matone ya umande wa
neema yanang'aa;
Angaza tu kunizunguka.

²⁰⁴ Ziondolee mbali nami hizi chemchemi za kujitengenezea! Sijui chemchemi nyingine; ila Damu Yake Yesu! Hiyo ndiyo Chemchemi pekee ninayotaka kujua. Acha Neno likae ndani yangu, Bwana; litie maji kwa Roho Wako.

²⁰⁵ Angalia, sasa, kama huyo Roho aliyemfufua Yesu kutoka kaburini, anakaa ndani yako, kwa uwezekano una Uzima; unaongozwa na Roho, kulihuisha Neno kwako, upate kuliadini Hilo. Kitu hicho kidogo kinaendelea kusukuma kinapokua.

²⁰⁶ Angalia, hapo Pentekoste, miili yao ilihuishwa kwenye Maisha mapya. Angalia kundi la maskini waoga.

²⁰⁷ Ninawachelewesha sana? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Angalieni, ndiyo kwanza tu nimepata nguvu, naam, najisikia vizuri. Loo, jamani!

208 Angalia, wao walikuwa waoga. Angalia. Bali, walikuwa na Mitambo. Mnaona? Bali wao wote walikuwa wameketi kule nyuma, wakisema, “Loo, mimi nawaogopa. Loo, ninaogopa kuondoka niende nikashuhudie, maana, loo, hao wote maaskofu wakubwa mno na kadhalika huko. Loo, ninaogopa kufanya hivyo. Hao makasisi na kadhalika, ninaogopa kushuhudia mambo hayo, naogopa nitasema nilimwamini Yeye. Loo, siwezi kufanya jambo hilo kamwe, mnaona?”

209 Lakini, mara moja, Nguvu za Utendaji zikaja. Ndiyo. Nazo zilifanya nini? Hazikuijaza tu roho yao, ndani, bali ziliihuisha Mitambo yao. Miili yao ilihuishwa. Hawakuwa waoga tena. Walitoka moja kwa moja kuwakabili watu uso kwa uso. Naam, bwana. “Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu!” Ambapo, kabla ya zile Nguvu za Utendaji hazijaja, wao walikuwa ni Mitambo tu. Mnaona? “Enyi watu mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu! Watu hawa hawakulewa, kama mnavyodhania.

210 Mimi ni mmoja wao. *Jambo hili* ndilo Lile! Nitawaonyesha ni nini. Ni Maandiko. *Jambo hili* ndilo lile! Nami daima nimesema, “Kama jambo *hili* silo *Lile*, acha nishikilie *hili* mpaka Lile litakapokuja.”

211 “La, jambo hili ni Lile lililonenwa na nabii Yoeli, ‘Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu.’” Mnaona, zile Nguvu za utendaji ziliingia katika ile mitambo. Hawakuogopa tena.

212 Baadhi yenu enyi watu ambao mnaogopa ya kwamba baadhi ya wanawake watawacheka kwa ajili ya kuwa na nywele ndefu, ama kuacha kujipodoa; baadhi yenu wanaume ambao mnaogopa ya kwamba madhehebu yenu yatawafukuza mkilibatiza kusanyiko lenu katika ubatizo wa Kimaandiko; mnapaswa kujifungia katika chumba cha juu hata Nguvu za Utendaji zitakapokuja. Hiyo ni kweli.

213 Ziliwabadilisha. Ziliwahuisha. Ziliwafanya taofauti. Wao walikuwa watu waliobadilika, tangu wakati huo na kuendelea. Ziliwahuisha, kutoka kwenye maisha ya kale ya kuwa mwoga, wakawa kama Simba wa kabila la Yuda. Wao walikabili kufia imani kabisa, wakaangikwa misalabani, wakasulubiwa kichwa chini miguu juu, wakachomwa moto, wakatupwa katika tundu la simba. Hakuna uoga tena, kwao. Mauti hayakuwa na ushindi juu yao, hata kidogo. Zile Nguvu za Utendaji zilikuwa katika ile mitambo. Naam, bwana. Ziliihuisha miili yao ipatikanayo na mauti.

214 Sasa sikilizeni. Hapa pana jambo lingine, kwa ushahidi. Ziliwahuisha sana kwa namna fulani hata (mwajua nini?) wao waliinuliwa juu katika ulimwengu wa Roho, na miili yao iliyo katika hali ya kufa ilihuishwa sana mpaka lugha yao ikabadilika. Zilininii tu... Hizo ziliihuisha lugha yao. Hivyo

ndivyo Biblia ilivyosema. Na, miili yao iliyo katika hali ya kufa ilipohuishwa, lugha yao ilihuishwa. Mawazo yao yakahuishwa. Roho zao zikahuishwa. Maisha yao yakahuishwa. Wao walihuishwa, kwa jumla! Walijaribu kuzungumza, nao hawakuweza kuzungumza katika lugha zo zote zile za kibinadamu. Wao walihuishwa sana katika Uwepo wa Mungu mpaka wakanena katika lugha mpya, lugha ya Kimbinguni. Whiu! Ni Nguvu za Kuhuisha za namna gani!

215 “Ikiwa Roho aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu,” loo, haleluya, “Yeye ataihuisha miili yenu ipatikanayo na mauti.” Atawafanya mfanye mambo ambayo hamkuyafanya hapo awali. Wao walikuwa wamejaa Nguvu za Kuhuisha wakati huo. Mnaona?

216 Mwili wako hauko chini ya dhambi tena; wewe, shauku zako.

Yeye anasema, “Njoo huku nje!”

Unasema, “Funga mdomo wako.”

“Loo, tuna ninii kubwa kuliko zote . . .”

“Funga mdomo wako.” Jamani, wewe ni tai!

217 Je! uliwahi kuona jinsi tai mzee anavyotembea kiungwana? Yeye harukiruki kama arukavyo koho, mnaona, kwenye kila ninii iliyokufa, na mizoga yote ilioozea ardhini. La, bwana. Yeye hutembea kwa fahari.

“Funga mdomo wako.”

“Loo, hiki hapa chakula kizuri cha jioni *hapa*.”

218 “Si kwangu mimi. Unaona, shauku zangu zimebadilika. Tamaa yangu ni tofauti. ‘Kwa kuwa mtu hataishi kwa mzoga uliooza wa dunia pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.’” Tai halisi aliyehuishwa huishi kwa jambo hilo. Amina!

219 Loo, Naye alimfufua Kristo kutoka kaburini, akiishi ndani yenu, amehuishwa miili yenu ipatikanayo na mauti katika Uwepo Wake. Unatambua jambo Hilo. Wewe si nderi tena. Wewe ni tai. Hutaki mambo ya dunia. Wewe ni mwana na binti wa Mungu. Unakula karamu kwenye chemchemi ambayo ulimwengu haujui kitu juu yake. Unamnywa Huyo. Mtu fulani anajua . . . Ulimwengu haujui kitu juu ya jambo hilo. Unakula Mana iliyofichwa ambayo ulimwengu hata haujawahi kujua kitu juu Yake, kwa maana wewe ni tai. Umehuishwa mahali ambapo unaweza kuifikia Hiyo. Huwezi kuifikia *hapa* chini, huna budi kuja *hapa* juu. Huna budi kuhuishwa, kuinuliwa juu kule, kusudi Hiyo ipate kuhuisha.

220 Walifanya nini? Walinena katika lugha nyingine. Biblia ilisema walinena. “Walineni katika kila lugha chini ya Mbingu.”

221 “Ungeweza kuwazia jambo hilo, hiyo miili mizee ipatikanayo na mauti iliyo mle, iseme, “Vema, sijui sasa kama naweza kuamini jambo hili au la.”?”

222 Mara, wao walihuishwa sana mpaka ule uhodari wa Simba wa kabila la Yuda ukashuka juu yao, juu ya huo Mganda wa kutikiswa. Loo, huyo Tai alikuja kuwaita walio Wake! “Nao hawakupenda maisha yao hata kufa.” Amina.

Na kutakuweko na wengine watakaotoa uhai wa damu yao.

Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na mafuriko Yake yaliyo mekundu sana.

223 Naye Mwana hana budi ku—kufunuliwa tena, ndani ya Bibi—arusi katika siku za mwisho; Nguvu za Kuhuisha hazina budi kuja, ziwahuishe kutoka kwenye madhehebu haya pamoja na kanuni za imani zilizokufa, waingie kwenye Neno lililo Hai la Mungu aliyehai. Loo!

224 La, liliwahuisha wakaingia kwenye Maisha mapya. Linafanya jambo lile lile kwetu sasa. Angalia, basi, wao walihuishwa sana katika hizo Nguvu za Kuhuisha! Sasa mimi. . .

Sikilizeni kwa makini sasa. Ninajaribu kuwaonyesha.

225 Zile Nguvu za Kuhuisha hazikuwa tu katika nafsi zao, bali ziliwajaa kila mahali. Hizo. . . Si kwamba tu Nguvu za Utendaji zilikuja ndani, kuhuisha, bali ziliihuisha ile mitambo. Mnaona ninalomaanisha? Walihuishwa sana hata ndimi zao zikaanza kunena katika lugha nyingine. Wao walihuishwa sana na Nguvu za kufufuka kwa Kristo, hata wakaweka mikono yao. . . Walihuishwa sana kwa Nguvu za kuhuisha, hata, walipoiweka mikono yao juu ya wagonjwa, walipata afya. “Zilihuisha mwili wako upatikanao na mauti.” Waliponywa, kwa kuwekewa mikono yao.

226 Naye Roho akauhuisha ushirika wao pamoja na Mungu, hata wao pia wakahuishwa sana katika Uwepo wa Mungu hata, wakati mtu alipokufa na nafsi yao ikawa imeondoka, Hizo zilimfufua tena. Amina! Utukufu! Sasa najisikia kubarikiwa.

227 Hiyo ni kweli, kuhuishwa! Si kwamba tu huo ufufuo ulikuwa kwa ajili Yake Mwenyewe, bali ni kwa ye yote atakaye, kwa Mzao huyu aliyechaguliwa tangu zamani aliyelala pale. Kuhuishwa, zinahuisha mwili upatikanao na mauti!

228 Wao waliwawekea wagonjwa mikono; wakapata afya. Waliomba; katika Roho waliona ono, wakawafufua wafu. Hiyo ni kweli. “Miili yao ipatikanayo na mauti ilihuishwa.”

229 Kama zikiingia ndani yako; kama itakuwa ninii sana... Sasa, unaweza kusema ndivyo ilivyo; bali kama ndivyo ilivyo, ishara hizi zitafuata jambo hilo, mnaona. "Zinauhoisha mwili wako upatikanao na mauti." Hizo zitakuhoisha.

330 Sasa, angalia, kuhuisha katika Uwepo wa Mungu. Kwa nini? Ilikuwa ni Roho wa Mungu aliyemfufua Yesu katika wafu. Na, Roho wa Mungu, "Ninawapa Uzima wa Milele," linatoka kwenye Neno la Kiyunani, kama ukilitazama, *Zoe*, ambaye anaupitisha Huo kwenu halafu unaihoisha (yao) hata nia zao.

231 Sasa angalia. Wawezaje kusema ya kwamba Roho huyo anaishi ndani yako? [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tano—Mh.] Ingawa ulifanya kila kitu ulichofikiria kilikuwa sawa, huu hapa ushuhuda wako kama unaye Huyo ama huna. Ikiwa Roho aliyekuwa katika Kristo anakaa ndani yako, Yeye pia anakuhisha kwenye Neno, kwa kuwa Yeye ni Neno. Na kama huyo, kinyume, anakuhisha ukaliacha Neno, basi huyo si Roho wa Kristo!... sijali uliyofanya, mpaka Huyo atakapokupeleka kwenye Neno. "Kondoo zangu wanaisikia Sauti Yangu, nao wataishi kwa kila Neno," kila Neno! Nilikuwa nikizungumzia jambo hilo juzijuzi.

232 Mama yangu mwenyewe, ameaga dunia sasa, naye alikuwa mwanamke wa ajabu sana. Naye alikuwa, mwajua, karibu nusu Mhindi, naye alikuwa wa ajabu. Bali mle ndani alikuwa mtu ambaye hakuota ndoto. Bali sifikiri... Yeye aliota ndoto nne ama tano, maishani mwake mwote. Bali kila alipoota ndoto, ilikuwa ni ya kweli. Alipoota ndoto, ilikuwa ya kweli.

233 Nakumbuka wakati mmoja nilipoanza kuhubiri kwa mara ya kwanza, miaka mingi iliyopita. Tulikuwa tunaishi papa hapa upande wa juu wa barabara, moja kwa moja karibu na upande wa juu wa mahali hapa. Nilikuwa nikihubiri papa hapa kwenye kanisa hili. Naye akaota ndoto, kwamba nilikuwa nimesimama hapa karibu na vipandio vitatu. Nami nilikuwa nimesimama, nikimhubiria kila mtu, ya kwamba hawana budi kupanda vipandio hivi vitatu kabla hawajafikia ile barabara kuu. Na kwenye hiyo barabara kuu kulikuweco na mstari mdogo mweupe kama lulu, ulioenda moja kwa moja hata kwe—kwe—kwenye milango ya Mbinguni, hata kwenye mlango wa lulu. Na hiyo lulu ilikuwa imetandazwa juu ya hivi vipandio. Kama huo si Ujumbe wangu hasa leo; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu! Nami nilikuwa nikisema ya kwamba mtu hana budi kupitia kwenye vipandio hivi vitatu, apate kutembea kwenye barabara hiyo kuu. Na nikasema ya kwamba... .

234 Akaja bibi mmoja. Sasa, mnajua watu walivaa viatu vya namna gani miaka thelathini na mitano iliyopita. Akaja bibi mmoja, alikuwa na viatu vyenye visigino virefu kama

wanavyovalia siku hizi, viatu vyenye visigino vilivyochongoka. Naye akapita pale. Ndipo nikasema, “Ngoja kidogo, dada. Huwezi kutembea kwenye hiyo barabara kuu ukiwa na hivyo.” Tena nikasema, “Wewe—wewe, huwezi kufanya jambo hilo.”

²³⁵ Naye akasema, “A-ha!” Akasema, akawageukia hao wanawake wengine, akasema, “Msimwamini. Yeye ni mwenda wazimu. Mnaona? Msimwamini. Nitawaonyesha naweza kuhesabiwa haki, nitakaswe, na nijazwe na Roho Mtakatifu, na bado nitembe kwenye vile.” Naye...Nikamwacha tu aende. Nisingeweza kufanya cha zaidi juu ya jambo hilo, nisingeweza kumkataza. Basi akaruka kwenye hiyo barabara kuu. Naye akaangalia nyuma kwa huyo dada, akasema, “Mnaona, niliwaambia!” Akaanza kupanda mbio, naye... .

²³⁶ Mnajua, kama ilivyosema Biblia, katika Isaya, sura ya 5, ya kwamba wangukuwa na “shingo zilizonyoshwa.” Hawana budi kuwa nazo; wao wameinama, mnaona. “Wakienenda kwa hatua za madaha...” Hawana budi kufanya hivyo, hawana budi kukatika viuno, “Wakienda kwa hatua za madaha, wakiliza njuga kwa miguu yao; mnaona, binti za Sayuni katika siku za mwisho.”

²³⁷ Naye akaanza kupanda ile barabara kuu, akitimua mbio alivyoweza kukimbia. Ndipo, baada ya muda kidogo, ile barabara ikaanza kuwa nyembamba zaidi na zaidi. Akaanza kupepesuka, kupiga hatua za madaha namna *hiyo*, na kisha akaanguka.

²³⁸ Ndipo mama akasema, “Makelele ya kutisha sana niliyopata kusikia maishani mwangu, yalikuwa ya huyo mwanamke anayeanguka kwenye miali hiyo ya moto na moshi, akianguka chini, chini namna hiyo.” Kasema, mimi “niligeuka nikasema, ‘Mnaona?’”

²³⁹ Yeye alitii tu kila kitu ila Neno moja, mnaona, kila kitu ila Neno moja. Hakika, wanawake wa Kipentekoste wanaweza kuokolewa, kutakaswa, na kujazwa na Roho Mtakatifu, kisha washindwe. Kweli kabisa. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo.” Mnaona? Mnaona? Naye akashindwa. Na kama nilivyosema, mnaona, angalienda mpaka aingie ndani, sawa, lakini, mnaona, alishindwa kusikiliza; kumwambia kilichokuwa hapo mbele. Naye ameandika Injili kwa njia ya wanafunzi, mitume, na Mafundisho ya mitume na manabii, na kadhalika, nao hawatasikiliza.

²⁴⁰ Sasa angalia Nguvu hii ya kuhuisha, *Zoe*, ikileta Neno, nia iliyokuwemo katika Kristo ilikuwa ndani yenu basi. Ninajaribu kuwaonyesha, ya kwamba, ninyi, mlipofufuka. Wakati Mungu alipomfufua Yesu katika wafu, Yeye aliwafufua ninyi, pia. Na pia mkahuishwa mpate Uzima, pamoja Naye, sasa mmepewa Uzima, ingawa wakati huo mlikuwa tu si kitu

ila sifa katika mawazo Yake, bali Mungu alikuwa ameona yote katika Yeye, pale mwisho, mnaona. Wakati Mungu alipoangalia chini katika ule mwili . . .

²⁴¹ Roho alimwacha Yeye, kwenye Bustani ya Gethsemane. Alipaswa kufa, akiwa mwanadamu. Kumbukeni, marafiki, haikumbidi kufanya jambo hilo. Huyu alikuwa ni Mungu. Mungu aliutia ule mwili mafuta, ambao ulikuwa ni mwili wa binadamu. Naye haikumbidi. . . Kama angalienda pale juu, kama Mungu, Yeye asingalikufa kifo cha namna ile kamwe; huwezi kumwua Mungu. Lakini haikumbidi kufanya jambo hilo.

²⁴² Lakini, kumbukeni, Yeye alienda pale huku ninyi mkiwa ndani Yake. Mnaona, Mungu hakuwa amemtenganisha Bibi-arusi kutoka kwa Bwana Arusi, bado. Kwa hiyo wakati Mungu alipoangalia chini kwenye mwili wa Kristo, Yeye aliona wa kiume na wa kike pia. Wote walikuwa wamekombolewa katika mwili huo mmoja. Mnaona? Wao ni mmoja, ni kitu kile kile, Neno lile lile. Neno lile lile, lililozungumza juu ya Bwana Arusi, linazungumza juu ya Bibi-arusi.

²⁴³ Vema, Bibi-arusi anawezaje kuja, na kushindwa kudhihirisha kila kitu alichohidiwa na Yeye; na Bwana Arusi amekuja, na asingekuwa Bibi-arusi? Bali wakati alipofanya kila kitu, hata kulithibitisha kwa kujifufua Mwenyewe katika wafu, baadaye, basi si—si Bibi-arusi atapaswa kufanya jambo lile lile, anapaswa kuwa kile hasa Neno lilichosema Yeye angekuwa katika siku hizi za mwisho? Yeye si anapaswa kurudi kupitia Malaki 4? Yeye si anapaswa kudhihirishwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma? Ulimwengu si unapaswa kuwa jinsi ulivyo hasa? Hivi mambo haya si ni utambulisho mkamilifu wa Neno la Mungu lililofunuliwa kwetu?

²⁴⁴ Vema, marafiki, ninajua ninawaweka muda mrefu, dakika kumi na tano kufikia wakati wa chakula cha mchana, lakini labda nitamaliza ifikapo wakati huo. Lakini angalieni, tazameni hapa, ni jambo kamilifu jinsi gani. Sijui nitakapowaona tena. Mnaona?

²⁴⁵ Angalia, chunguza jambo hili. Bali Mungu alimwona Bibi-arusi akiwa ndani ya Bwana Arusi. Haleluya! Mnaona, kumwoko Mke Wake, kama Adamu, ilimbidi kwenda pamoja Naye. Adamu alijua alichokuwa anafanya; Hawa hakujua alichokuwa anafanya, bali Adamu aliondoka na mkewe. Mnaona? Naye Yesu alipachukua mahali pa Mke Wake na akafanyika dhambi kwa ajili Yake. Kumbuka, Yeye alifanyika wewe, Yeye aliistahimili adhabu yako, kusudi upate kusimama mahali Pake. Alisimama mahali pako, upate kusimama mahali Pake. Ni upendo wa jinsi gani! Ni ushirika wa jinsi gani!

Tunawezaje kuukana? Tunawezaje kufanya lo lote ila kumpenda Yeye, ewe rafiki? Ningeweza kudumu kwa jambo hilo masaa kadha, bali hebu tusonge mbele kidogo.

²⁴⁶ Kama vile lile tukio la Kipentekoste leo, na kule kuja kwa Roho Mtakafifu katika siku hizi za mwisho, kama ilivyoahidiwa, ni kama vile thibitisho lilivyo kwa hati ya kumiliki. Mnaona?

²⁴⁷ Sasa, unaweza ukapata hati ya kumiliki. Hakika. Mnaona? Unaweza kupata hati ya kumiliki ya mahali fulani, bali hiyo bado haimaanishi ya kwamba ni yako. La, bwana. Mtu mwingine kutoka huko mbali sana anaweza kuja na kupadai. Bali unapopata lile thibitisho, hilo linaonyesha ya kwamba kila kitu ambacho kimewahi kuwa dhidi yake kimeondolewa, moja kwa moja tangu kwenye msingi. Sivyo?

²⁴⁸ Na wakati mtu amesema ya kwamba anaamini Neno, na halafu Roho Mtakatifu anapokuja, Ndiye ile hati. Nalo linakupa ruhusa, unapokuwa na hilo thibitisho, ya kwamba kila sehemu ya kitu hicho ni Mali yako, na kila kitu kilicho juu yake ni chako. Amina! [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tatu—Mh.] Na jambo hilo linatupa lile thibitisho, wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu ya hati hii ya kumiliki ambayo Mungu aliiona huko nyuma kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kuliweka jina katika Kitabu cha Uzima; bali ulizaliwa kupitia kwa mwanamume na mwanamke, na unaweza kutenda dhambi, na una hatia ya dhambi. Bali wakati nilipoliamini Hilo, nilipata ile hati; bali wakati Roho Mtakatifu alipokuja, ilikuwa ni thibitisho kwamba kila kitu kilichokuwa dhidi yangu, kama mama yangu alikifanya, baba yangu alikifanya, nyanya yangu alikifanya . . .

²⁴⁹ Kama yule mtoto mdogo mwenye kifafa niliyemwombea, dakika chache zilizopita, kilichokuja kupitia kwa babu na nyanya zake. Hicho kifafa kilishuka chini, na kuja juu ya huyo mtoto, nilisema.

²⁵⁰ Bali wakati thibitisho limekuja, lilifutilia mbali, likasamehe kila kitu. Mimi ninalo lile thibitisho basi. Amina! Na kama vile kweli Roho alivyomfufua Kristo katika wafu, mimi nina Thibitisho la hiyo hati ya kwamba mimi ni sehemu ya Mwili huo, nikiwa na thibitisho la Roho Mtakatifu likiufanya mwili huo wa Neno kuishi kama vile tu Yeye alivyoishi katika Yeye, kama alivyoahidi katika siku za mwisho. [Ndugu Branham aligonga mimbara mara nne—Mh.] Lile thibitisho! Dhambi zangu zote zimefutuliwa mbali, dhambi zako zote zimefutuliwa mbali, na Damu ya Yesu Kristo, Naye Roho Mtakatifu amekuja kama thibitisho la hati ya kumiliki ambayo Mungu alinipa kwa neema, kwa kujua tangu zamani. Loo, jamani!

251 Mnaogopa nini? Si ajabu Yeye alisema, “Msiogope; Ndimi niliyekuwa nimekufa Nami ni hai tena; Nami ni hai milele hata milele; na ninazo funguo za mauti na kuzimu.” Msijali kitu. Hata mauti hayatawadhuru. Angalieni. Inapendeza sana!

Hebu tuharakishe sana sasa.

252 Thibitisho la hati ya umilkaji! Deni imelipwa. Kila kitu kilicho dhidi yake kimefutuliwa mbali. Ha-ha-ha! Utukufu! Huenda nikatenda kama punguani, bali ninajisikia vizuri. Angalieni. Mnaona? Loo, thibitisho la hati ya kumiliki, unatambua jambo hilo linamaanisha nini? Unatambua jambo hilo linamaanisha nini, ndugu? Hakuna kinachoweza kuuondoa kwako. Amina. Mimi ninalo. Amina. Ni. . .

253 Hati gani? Sasa nimechukua urithi wangu, wa kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Yeye alifanyika mimi, ili nipate kufanyika Yeye. Sasa, Yeye alifanyika mwenye dhambi, ili nipate kufanyika mwana, amina, na kushika lile thibitisho la hati. “Kwa maana ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” mnaona, thibitisho la hati.!

Sasa upesi, kabla. . . Tuna kama dakika kumi zaidi.

254 Hebu sasa tuangalie, upesi, kule kuhuisha kwa Roho. Nitawaonyesha ishara fulani ili kwamba mpate kuelewa. Angalieni, sasa angalieni kile, hii “nguvu ya kuhuisha” ilikuwa ndilo somo langu. Baada ya Mwana kufufuka, angalia jinsi ilivyofanya kwao pale Pentekoste, kile ilichowafanyia, kile Nguvu hizo za kuhuisha zilichowafanyia. Ziliwahuisha.

255 Basi hebu tuone zilivyomfanyia Stefano. Stefano alikuwa amejaa Nguvu za kuhuisha. Hiyo si ilikuwa ni kweli? Mnaona, yeye alikuwa amejaa Nguvu za kuhuisha. Hizo zilimfanyia asiogope. Yeye alisema, “Enyi wenye shingo gumu na msiotahiriwa mioyo wala maskio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo. Ni yupi kati ya manabii waliotabiri kuja Kwake yule Mwenye Haki, ambaye baba zenu hawakumpiga mawe?” Loo, jamani! Zilimfanyia kitu fulani. Hakika, Yeye alikuwa amejaa Nguvu za kuhuisha.

Nao wakasema, “Tutamwangamiza jamaa yule!”

256 Na wakati alipokufa, wao walimpiga mawe; na maskini kichwa chake, mawe yakikipiga namna hiyo. Aliangalia juu akasema, “Naona Mbingu zimefunguka.” Nguvu za kuhuisha zilikuwa zikitenda kazi. “Naona Mbingu zimefunguka, na Yesu amesimama upande wa mkono wa kume wa Mungu.” Hivyo ndivyo zile Nguvu za kuhuisha zilivyomfanyia Stefano.

257 Angalia jamaa mwingine, aliyekuwa na hizi Nguvu za kuhuisha, jina lake lilikuwa Filipo. Alikuwa amejaa sana Nguvu za kuhuisha. Alikuwa na mkutano mzuri mkubwa huko Samaria. Pepo walikuwa wanatolewa. Watu walibatizwa

katika Jina Yesu Kristo. Walikuwa na mkutano halisi kweli. Kisha Roho akanena naye, loo, zile—zile Nguvu za Utendaji zikashuka, Nazo zikasema, “Ondoka kwenye ufufuo huu.” Lakini wahudumu watasema nini? Haidhuru watasema nini. Mnaona? Yeye alikuwa amejaa Nguvu za kuhuisha. Alikuwa na petroli, na—na Nguvu za Utendaji zilikuwa zikishuka juu yake. Kasema, “Nenda kule jangwani.”

²⁵⁸ Naye akakutana na towashi kule, na akambatiza katika Jina la Yesu Kristo; mtu mmoja, aliyeupeleka Ujumbe huko Kushi. Hiyo ni kweli? Naye akamtii Mungu.

²⁵⁹ Katika kumtii Mungu, kama hujawahi kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, fanya hivyo, kisha uone Nguvu za kuhuisha zikikuchukua basi. Mnaona?

²⁶⁰ Stefano alipofanya jambo hili kuu. . . ama, si Stefano. Bali Filipino alipofanya jambo hili kuu, kuondoka kwenye ufufuo huo mkuu na kutii amri za Mungu, wakati alipotimiza, kwa. . . Kwa kumbatiza towashi huyu, katika kumtii Mungu, yeye alijaa sana zile Nguvu za kuhuisha hata zikamtwaa. [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.] “Zitaihuisha miili yenu ipatikanayo na mauti, kama Roho huyu aliyemfufua Kristo katika wafu.” Zilimhuisha Filipino hata hakuonekana kwa labda maili mia moja na hamsini, mahali pengine, katika nchi nyingine. Zilihuisha mwili wake upatikanayo na mauti. Yeye alifanya jambo hilo namna gani? Alikuwa amejaa sana Nguvu za kuhuisha.

²⁶¹ Loo, enyi Kanisa la Mungu aliye hai, hatuwezi kusimama hapa kwenye matiti madogo ya sukari tunayonyonya hapa leo. Hatuna budi kuwa tumejaa na kuomba vya kutosha, pamoja na Nguvu za kuhuishwa, mpaka kule kuhuisha kwa Roho Mtakatifu! Hatuna budi kunyakuliwa, siku moja, katika kule Kunyakuliwa huko ng’ambo. Naam, bwana. Amina! Loo, jamani!

²⁶² Samahani kwa tamshi hilo. Nilikuwa nikifikiria juu ya mama anayetengeneza hivyo vijifuko vidogo, tulikuwa tunavitengeneza, kwa ajili ya mtoto mchanga. Baadhi yenu mama wa zamani mnakumbuka. Maskini mtoto mchanga anaanza kulia; unachukua kahawa kidogo iliyosagwa pamoja na sukari kidogo, unaifunga katika kijifuko na kumwacha akinyonye, kumtuliza tu. Hakuna nguvu katika hiyo. Itamwua. Mnaona? Hiyo sumu ya kale ya kahawa mle ndani, na kadhalika, imetiwa sukari kidogo kumfanya aimeze, inamtia sumu ya kahawa.

²⁶³ Tumechoshwa na upuuzi kama huo. Rudini! Ninyi ni tai; rudini kwenye Neno la Mungu! Iweni washupavu; hakuna kinachoweza kuwaudhi, kwa hiyo ninyi ni huru na kashifa yote ya mwanadamu. Hata mtu ye yote aseme nini juu yenu, jambo hilo huleta tu upendo mwingi zaidi. Amina. Na, Nguvu

za kuhuisha, mmenyakuliwa hata Mbinguni, tai ambaye tayari ameruka juu ya kuku, kule juu kabisa katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. Loo!

Hizo zilikuwa juu ya Filipo. Ambazo zilimhuisha, na kumtwa.

²⁶⁴ Hebu tumchukue mtu mwingine. Kulikuweco na mtu jina lake Henoko. Sasa, yeye tayari alikuwa ametembea na kila Neno la Mungu, kwa yapata miaka mia tano. Alikuwa na ushuhuda, ya kwamba, “Mimi sijalikosea Neno Lake hata wakati mmoja.” Yeye alijaa sana ile Nguvu ya kuhuisha wakati zile Nguvu za Utendaji zilipomgusa, kwenye hiyo Mitambo, hata haikumpasa kufa; aliondoka tu akaenda zake nyumbani. Alianza tu kutembea. Yeye alikuwa ninii sana. . . Kama Filipo, alijaa sana zile Nguvu za kuhuisha, badala ya kwenda Gaza na kwenda mahali pengine, ambapo, walikutana naye kwenye nchi za juu kule. Badala ya njia hiyo, yeye alienda tu, loo, akasema, “Mimi ni mzee, hata hivyo. Nina kiasi fulani tu cha Nguvu za kuhuisha, nitatembea tu niondoke ulimwenguni.”

²⁶⁵ Hizo ndizo Nguvu zile zile za Kuhuisha tulizo nazo sasa hivi. Mnaona, Hizo zitaihuisha miili yenu ipatikanayo na mauti. Sivo? Ni zile Nguvu za kuhuisha.

²⁶⁶ Henoko, akiwa na ushuhuda huo mkamilifu, ya kwamba, “Kila kitu alichoniambia Mungu nifanye, nilikifanya. Kila kitu nilichoona amesema nifanye, nilikifanya.” Naye a—akajaa sana Nguvu za Utendaji, ama—ama Mitambo, hata, wakati Nguvu za kuhuisha zilipomgusa, ile Mitambo, zilimwinua moja kwa moja juu. Alitembea moja kwa moja akatoka duniani, akaingia Mbinguni.

²⁶⁷ Sasa, sasa angalia. Juu ya Eliya, baada. . . Angalia, Eliya, huyo nabii mkuu, mtu katika siku zake. Samahani. Ndugu, dada, katika siku hiyo aliyokuwa amewakemea hao wanawake waliojipodoa nyuso zao, hao Mayezebeli na akina Ahabu, kisha akasimama mpaka. . . Na hakuna mtu, ilivyoonekana, aliyesimama pamoja naye. Naye alikemea, na kuwakazia macho, na kusimama kule nje, naye Mungu alikuwa amemwangalia na kumsaidia katika kila mahali. Mwajua, maskini mzee huyo alichoka siku moja. Akasema, “Ninazeeka, kwa hiyo siwezi kwenda mbele zaidi.” Alikuwa anaelekea, nakisia, umri wa miaka tisini; mzee sana, na akitembea kila mahali pale, naye alikuwa amejaa sana Nguvu za kuhuisha. Mwajua nini? Aliangalia ng’ambo ya Yordani.

Ee Mungu! Karibu naweza kuona ng’ambo ya pili. Nanyi je?

²⁶⁸ Alikuwa amejaa sana Nguvu za kuhuisha, hata, akaona gari limefungwa pale, baadhi ya farasi wa Moto na gari la Moto, wamefungiwa kwenye mti fulani kule. Yeye alivuka tu

ule mto akaenda nyumbani, bila hata ya kufa. Nguvu za Kuhuisha zilituma, zilisababisha gari kushuka kutoka Mbinguni likamnyakua. Hata waliokota koti lake wakamtupia Eliya. Hiyo ni kweli.

²⁶⁹ Naam, ndipo jamaa huyo akalitwaa joho hilo, mfano wa Kanisa tena, mnaona, akaliokota lile joho. Sasa, yeye alifanya miujiza maradufu, jambo ambalo ni mfano wa Kristo na Kanisa. Mnaona? Eliya alifanya minne; yeye akafanya minane. Mnaona, sasa, yeye alikuwa—alikuwa na nguvu maradufu, maana aliziomba. “Mambo mengi kuliko haya ninayofanya Mimi nanyi mtayafanya.” Mnaona? Bali yeye alikuwa amejaa sana Nguvu za kuhuisha, na kila kitu, hata akafanya haya yote, maradufu ya aliyofanya Elisha, kuliko aliyofanya. Basi angalia, yeye aliishi akafikia umri wa miaka themanini ama tisini, akawa mzee kisha a—akafa. Yeye alikufa, nao—nao wakamchukua wakamzika.

²⁷⁰ Unajua, vema, Nguvu hizo za kuhuisha hazikumwacha. Miaka mingi, mingi sana baadaye, wakati nyama zote zilikuwa zimeoza zikatoka kwenye mifupa yake, yeye alikuwa amelala kaburini. Nao walikuwa wamebeba maiti siku moja, ndipo wakamwona adui, basi wakamtupa mtu huyu mle ndani juu ya mifupa ya Elisha. Kulikuweko na Nguvu nyingi sana za kuhuisha katika mifupa hiyo hata mtu huyo akaruka akawa hai tena. Loo!

²⁷¹ “Huyo atauhuisha mwili wako upatikanao na mauti.” Ingawa umekufa na kuoza kaburini, hata hivyo Nguvu hizo za kuhuisha zilitulia juu ya hayo mavumbi. Haleluya! Uhm! “Yeye aliyemfufua Kristo katika wafu pia huuhuisha mwili wako upatikanao na mauti.” Yule Eliya kule nyuma, Elisha na Eliya . . .

²⁷² Kumbuka, mtu huyo aliyekuwa amekufa, nabii huyo, aliyejaa Nguvu hizo za Kuhuisha, amelala kaburini na kuoza; kulikuwako na Nguvu nyingi sana za kuhuisha, hata, walimtupa mtu aliyekufa juu yake, akafufuka. Yeye bado angeweka mikono yake juu ya wagonjwa. Sivyo? Amina! Haya basi.

²⁷³ Basi kumbukeni, sisi ni mwili wa mwili Wake, Yesu Kristo. “Sisi ni mwili wa mwili Wake, na mfupa wa mifupa Yake.” Loo, hakuna njia ya kuliepuka. Sisi tutafufuka, na ni hayo tu. Utafufuka tu, hilo tu.

²⁷⁴ Pasaka inamaanisha zaidi ya mapokeo. Ndivyo ilivyo sasa pia, kwa kuwa miili yetu imehuishwa pamoja Naye nasi tumeketi katika ulimwengu wa Roho.

²⁷⁵ Na yewezekana huu uozee baharini; yewezekana uozee ardhini; yawezekana kusiwe na kijiko kimoja cha jivu; bali utafufuka. Kwa maana, Roho aliyemfufua Bwana wangu katika wafu amehuisha mwili huu upatikanao na mauti.

Ameuhuisha mwili wako upatikanao na mauti. Nasi ni warithi Wake wa kufufuka Kwake, bima Yake ya Uzima wa Milele ninayonena sana habari zake, mwajua. Si ajabu Yeye alisema, “Msiogope.” Yeye angejua.

²⁷⁶ Kwa kuwa kama Paulo alivyosema, “Mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, ku wapi kushinda kwako? Mimi nimejaa sana Nguvu za kuhuisha. Mungu ashukuriwe, atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Ndio, bwana! Nguvu za kuhuisha. Loo, jamani!

²⁷⁷ Yeye yu hai milele na milele, “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Waebrania 13:8. Angalia, Masihi, Mtiwa Mafuta; vivyo hivyo Bibi-arusi Wake, hao Masihi wadogo, mnaona, Mtiwa mafuta.

²⁷⁸ Angalia, Mauti haizizuii Nguvu za Mungu za kuhuisha. Mauti hayawezi kuzizuia Hizo. Unapokuwa Nazo, ni za Milele. Hakuna kitu kitakachozizuia Hizo. Huwezi kuzizuia; huwezi—huwezi kuzifanya cho chote. Ukimaliza maisha yako, hilo bado halizizuii; zina nguvu tu kama zilivyokuwa.

²⁷⁹ Angalia, Musa amejaa Nguvu hizo za kuhuisha. Sivyo? Yeye alikuwa nabii ambaye Neno lilimjia. Alikuwa sehemu ya Neno. Alikuwa Neno la siku hiyo. Hiyo ni kweli? Na baada ya kufa, miaka mia nane; kwenye Mlima wa Kugeuzwa, huyo hapo amesimama, pamoja na Elisha. Hiyo ni kweli? Nguvu za kuhuisha, mauti kamwe hayaziondoi. La, la. “Nitamfufua tena.” Malaika walikuja; wakamzika kule chini bondeni. Alikuwa ameoza na amekwisha, mifupa yake ilikuwa imekwisha, na kila kitu kingine, bali zile Nguvu za kuhuisha zilikuwa zingalipo. Zilimhuisha na kumfufua. Naye yule pale, amesimama pale. Angalia.

²⁸⁰ Mnasema, “Hiyo ni kweli, Ndugu Branham, baada ya miaka mia nane?” Loo, jamani!

²⁸¹ Kama ungesoma katika Mathayo, nina Andiko hapa, Mathayo 27:51. Mnaweza kuliandika, liandikeni. Wakati hao wote huko nyuma, walioamini ya kwamba Yeye angekuja. . . Biblia ilisema hapa, baada ya Yeye kuja, wao walikuwa wamelala mauti ardhini. Nguvu za kuhuisha zilikuwa juu yao, nao walikuwa sehemu Yake, hao watakatifu. Walikuwa sehemu Yake, kwa maana walikuwa wamemwamini Yeye.

²⁸² Kwa uwezekano walikuwa na huo Uzima, kwa dhabihu ile ya kondoo, upatanisho, ambayo isingeweza kamwe kuleta roho ya kondoo juu ya huyo mtu. Vipi sasa kukiweko na Roho ya huyo Mtu, Mungu Mwenyewe, juu Yake, mnaona, tuna Nguvu za kuhuisha kiasi gani zaidi! Lakini kwa upatanisho kwa ajili ya dhambi alitolewa mwana-kondoo, katika mfano. Tulio nao si mfano; bali ni mfano wa mfano. Tunaogopa nini? Na jamaa hao ambao walikuwa tu na mfano, ulioelekeza kwenye kufufuka Kwake, na wakaenda kaburini nao.

283 Kama Ayubu nyuma huko chini ya kuhangaika kwake kukuu, jamani, kila kitu kiliondolewa kwake! Ibilisi alisema, “Hebu nimtie mikononi. Nitamfanya akukufuru Wewe usoni Pako.” Na ndipo yeye akapata nafasi.

284 Akasema, “Usiuchukue uhai wake.” Naye (yeye) alifanya yote ila kuutwaa uhai wake.

285 Na mkewe hata alimgeuka. Akasema pumzi yake ilikuwa ng’eni kwake. Kwa maneno mengine, yeye—yeye asingekuwa na uhusiano wo wote naye. Hakuonekana kana kwamba anampenda tena, alimsukumia mbali tu. “Ayubu, wewe uko katika hali mbaya sana! Mbona usimkufuru Mungu, ukafe?”

Kasema, “Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu.” Loo, jamani.

286 Mnaona, yeye alishikilia moja kwa moja kile alichokuwa nacho. Sasa, yeye alikuwa nabii. Alisema, “Mimi si mwenye dhambi. Nimetoa dhabihu iliyoandaliwa.” Amina. Yeye alijua mahali alipokuwa amesimama. Alikuwa kwenye Neno. Haidhuru hao wengine walisema nini, yeye alikuwa papo hapo kwenye Neno. Halafu hiyo saa kuu inayotisha sana. . . Kasema, “Unanena kama mwanamke mpumbavu.” Akasema, “Bwana alitoa, Bwana ametwaa; mbona, Jina la Bwana na libarikiwe!” Kasema, “Mimi nilikuja katika ulimwengu huu bila kitu. Nilikuja hapa, nili uchi, nitaondoka vivyo hivyo. Jina la Bwana libarikiwe!” Ameketi pale, amejaa majipu, watoto wake wamekufa, alikuwa ameshikwa na umaskini, na marafiki wake wote wakamgeuka, washiriki wake wa kanisa, cho chote kile, akijikuna kwa. . . na jinsi gani alikuwa mwenye hali mbaya ya kutisha! Hakuna mmoja wenu aliyewahi kupitia katika hayo bado. Hata hivyo, yeye alishikilia kwenye hilo Neno.

287 Alikuwa tai. Loo, jamani! Huwezi kutanda utando machoni mwake kila wakati. La, la! Mara, akisimama kwenye hilo Neno, ni nini kilitukia? Anga zikawa nyeusi kabisa, ngurumo zikaanza kunguruma, umeme ukaanza kumulika, ndipo Ayubu akaangalia juu na kuona ono lile, kasema, “Najua Mteteaji wangu yu hai. Katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi hii. Na ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, mifupa na kila kitu, hizo Nguvu za kuhuisha zitakuwa pale. Mimi mwenyewe nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona kwa nafsi yangu. Macho yangu yatamtazama wala si mwingine.” Hiyo ni kweli? “Hata baada ya mafigo yangu kuliwa ndani yangu, hata baada ya mabuu ya ngozini yaliyo ndani ya mwili wangu sasa, yatauangamiza.”

288 Mwajua, mabuu ya ngozini hayakujii. Mabuu hayo tayari yamo ndani yako, mabuu yako mwenyewe ya ngozini. Ulipata kutambua jambo hilo? Wakutie kwenye sanduku, na walizibe

kabisa hewa isiweze kupenya; mabuu yatakukula wewe, vile vile, maana yamo ndani yako. Wewe ni lundo tu la wadudu, kwanza, ndani yako.

²⁸⁹ “Hata mabuu ya ngozini, mabuu yangu ya ngozini yakiniangamiza, mwili wangu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.”

²⁹⁰ Na kwenye asubuhi hiyo ya kufufuka! Utukufu! Haleluya! Mathayo, mwandishi huyu mkuu, 27:51, alisema, “Baada ya kufufuka katika wafu, ya kwamba watakatifu wa Agano la Kale, wengi wa hao waliolala katika mavumbi ya nchi, walifufuka kutoka kaburini, wakaingia mjini na kuwatokea wengi.” Hizo Nguvu za kuhuisha, zilikuwa bado zingali kwenye mifupa hiyo ya Eliya wakati hapakuwepo na mifupa tena, zilikuwa zingali katika Ayubu wakati hapakuwepo na kijiko kimoja cha mavumbi yaliyosalia ya mwili wake. Bali Nguvu hizo za kuhuisha zilikuwa zingali pale.

²⁹¹ “Kama Roho huyu aliyemfufua Yesu katika wafu akiishi ndani yako, Yeye atauhuisha mwili wako upatikanao na mauti.” Angalia, upesi sasa.

²⁹² Unasema, “Lo, laiti ningaliishi kule nyuma...” Unaiishi katika wakati mzuri zaidi. Sasa kama ninyi nyote...

²⁹³ Ninawaona mkiandika Maandiko. Vema, andikeni I Wathesalonike 4:16. Angalia jinsi linavyopendeza, mnaona. Katika wale... “Watakatifu, hao waliolala katika Kristo, Mungu atawaleta pamoja Naye,” mnaona, watakatifu walio kaburini, wakipumzika. Kama Eliya alivyokuwa; wengine kama alivyokuwa Elisha; mnaona, wengine wao watahuishwa, wengine wao watanyakuliwa, wengine watakuwa kaburini. Wataenda pamoja Naye. “Parapanda ya Mungu italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, kumlaki Bwana hewani.” Zile Nguvu za kuhuisha juu ya walio hai; zile Nguvu za kuhuisha juu ya waliokufa. Mnaona?

²⁹⁴ Nguvu zizo hizo za Kuhuisha za Mungu zikionyeshwa katika manabii hawa wawili. Angalieni majina yao, ni karibu sawa, Elisha, Eliya. Mnaona Bibi-arusi na Bwana Arusi? Mmoja wao ni Bw. Yesu; huyo mwingine ni Bibi Yesu. Mnaona, karibu sawa, ni—ni kati tu ya—ya Mwanamume na Mwanamke. Mnaona?

²⁹⁵ Eliya, basi angalia jinsi ilivyowakilishwa. Sasa, Elisha... Alitwaliwa juu katika kunyakuliwa, analiwakilisha Kanisa, vema, Eliya; naye Elisha alipumzika hata kwenye ufufuo. Mnaona? Ni kama tu vile ndege, anavyohitaji mabawa mawili kujiweka sawasawa. Mnaona? Kanisa liliwakilishwa papo hapo katika hao manabii wawili. “Kwa maana sisi tulio hai na tuliosalia hata kuja Kwake Bwana, hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti; kwa kuwa Parapanda ya Mungu

italia,” hayo mabawa mawili yataungana, nasi tutaruka twende, haleluya, tutaruka twende. Sababu, (gani?) katika walio hai, ama waliokufa, hizo Nguvu za kuhuisha zingali zinaishi.

²⁹⁶ Angalieni. Kumbukeni, kumbukeni sasa, kuhuishwa kuona mambo haya ni nini. Angalieni Nguvu za kuhuisha za siku hii. Kumbukeni, sisi tumehuishwa. Si muda mrefu uliopita, kwa ajili ya msaada . . .

²⁹⁷ Nami—nami nafikiri Bwana wetu alisema, na Paulo vile vile, “Aliyonionyesha Baba, sijawaficha lo lote. Mimi huwaambia.” Na katika siku hizi za mwisho ambapo tumeziona Nguvu Zake za kuhuisha juu yetu, Yeye hata alitupa sisi Nguvu za kuhuisha, kuona wagonjwa wakiponywa. Tumeziona Nguvu za kuhuisha zikitenda kazi miongoni mwetu, kama ilivyokuwa wakati huo juu yao katika siku za mwanzoni, mnaona, tunazona zikileta kwa ono na kuwafufua wafu, tunazona zikiwaponya wagonjwa.

²⁹⁸ Juzijuzi nilikuwa nikimwambia mtu fulani. Maskini Donovan Weerts hapa, nafikiri nyote mnamjua. Nilikuwa kule juu nikiwinda pamoja naye. Maskini jamaa yule . . . Yeye ni maskini jamaa mzuri. Huja hapa kanisani, ni rafiki yangu mwema. Naye tu . . . Alisema, “Sikutaka kukusumbua.”

²⁹⁹ Nikaangalia, na sikio lake, lote limetoka, upande wa ndani umetoka. Nami nikasema, “U hali gani, Donovan?” Nikamshika tu mkono, namna *hiyo*, na kansa. Nikasema, “Donovan, vipi sikio lako?”

³⁰⁰ Akasema, “Sijui, Ndugu Branham. Yapata miezi sita, saba, na linaendelea tu kuwa . . .”

Nikasema, “Mbona hukusema kitu juu yake?”

³⁰¹ Kasema, “Si—sikutaka kukusumbua, Ndugu Branham.” Nikasema, “Unajua ni nini?”

Kasema, “Nina fununu.”

³⁰² Niliweka tu mkono wangu juu yake, sikusema kitu. Siku mbili baadaye, hapakuwepo hata na kovu. Ni nini? Nguvu za kuhuisha, mnaona, zitauhuisha mwili wako upatikanao na mauti. Sikio lake lingeliwa, ubongo wake ungeangamia, mnaona, yeye angekufa. Lakini, zile Nguvu za kuhuisha! Mnaona?

³⁰³ Na siku moja nilipokuwa nimechoka, mwenyewe, juu ya . . . Nilisema, “Kama wewe . . . Kijana, afadhali uendele, una umri wa miaka hamsini. Wewe, kama utamfanyia Bwana lo lote, afadhali uharakishe kulifanya. Unazeeka.” Mnaona? Ndipo pale asubuhi ile, zile Nguvu za kuhuisha zikaja, Naye akaniruhusu niangalie ng’ambo ya pazia, nami nikawaona ninyi nyote kule ng’ambo. A-ha. Mnaona? Yeye akasema, “Kila

ulichowahi kupenda, na kila kilichowahi kukupenda, umepewa wewe.” Mnaona? Niliwaona hao kila mahali pale namna hiyo. Ilikuwa nini? Nguvu za kuhuisha.

304 Yohana Mfunuzi alijazwa Nguvu za kuhuisha, naye akasimama akaona mwisho kutoka mwanzo.

305 Isaya alikuwa amejaa Nguvu za kuhuisha, naye akasimama akaona ule Utawala wa Miaka Elfu na mambo yote.

306 Nguvu za kuhuisha! “Basi ikiwa Roho aliyemfufua Kristo katika wafu anakaa ndani yako, Yeye atauhuisha mwili wako ulio katika hali ya kufa...mwili upatikanao na mauti.” Kumbukeni, Nguvu za kuhuisha!

307 Angalieni kile tulichoona katika siku hii. Nguvu za kuhuisha zimekuja kwetu, kuzifungua zile Muhuri Saba. Hiyo ilikuwa nini? Akili ya mwanadamu? La, Nguvu za kuhuisha za Mungu. Mnaona, Nguvu za kuhuisha za Mungu zilitabiri jambo hili lingetimia. Mnaona, Nguvu za kuhuisha za Mungu ziliufanya ulimwengu uzishuhudie Hizo, ni Kweli. Malaika wa Bwana, niliwaambia, alikuwa hapa katika ile Nguzo ya Moto; Nguvu za kuhuisha ziliruhusu ulimwengu kushuhudia ya kwamba ni Kweli. Na, katika jambo hilo, wao hawakujua Hiyo ilikuwa ni nini; nasi tulijua, hebu angalieni upande *huu*, na ni Bwana wetu kule juu, mnaona.

308 Yeye ndiye aliyezifungua Muhuri hizo. Yeye ndiye Muhuri hizo, kwa maana Neno lote la Mungu ni Kristo, naye Kristo ndiye zile Muhuri zilizofunguliwa. Kule kufunguliwa kwa zile Muhuri ni nini basi? Kumfunua Kristo.

309 Na wale Malaika saba hasa, ambao waliyawakilisha yale Makanisa Saba yakikamilika yote, nasi hata hatungeweza kuliona jambo Hilo. Wao walifanya jambo hilo, walipiga ile picha, si sisi. Basi Ndiye Huyo hapo, amesimama pale, Hakimu Mkuu; akionyesha ya kwamba Yeye ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho. Ni thibitisho la jinsi gani! Nguvu za kuhuisha zilitutendea jambo hilo.

310 Nguvu za kuhuisha zinatufanya tuone kuja Kwake. Nguvu za kuhuisha zilitunyakua kutoka mautini tukaingia Uzimani. Nguvu za kuhuisha hutupa utambuzi; kujua una kasoro gani wewe, na la kufanya; yale uliyofanya, na yale hukupaswa kufanya; yale uliyopaswa kufanya, na kile utakachokuwa. Nguvu za kuhuisha, mambo yote haya!

311 Bwana wetu Yesu amejaa sana Nguvu za kuhuisha, Yeye alikuwa Hizo zote, pamoja. Yeye alikuwa amejaa sana Nguvu za kuhuisha, alisema jambo hili, “Uharibuni mwili huu, nami katika siku tatu nitausimamisha.” Nena kuhusu ujasiri katika Nguvu za kuhuisha! “Uharibuni mwili huu, nami nita... hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha.”

312 Kwa nini? Kwa nini angesema hivyo? Alijua ya kwamba ilikuwa imeandikwa juu Yake, mnaona, ya kwamba iliandikwa juu Yake, na Neno la Mungu ambalo lisingeweza kushindwa. Neno lilisema, “Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi yake katika kuzimu.” Naye alijua ya kwamba Nguvu za kuhuisha zingemfufua, ya kwamba kusingekuwa na chembechembe moja iliyoharibika.

313 Yeye alisema, “Liharibuni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalirudisha tena.”

314 Kwa nini? Ilikuwa ni unabii, Neno la Mungu. Na unabii, kama ni Neno la Mungu la kweli, hauwezi kushindwa. Basi unabii ule ule na Neno la Mungu lililosema Yeye angemfufua, linasema ya kwamba sisi tayari tumefufuliwa pamoja Naye. Si ajabu Yeye alisema, “Msiogope.” Pia imeandikwa, ya kwamba, “Roho ambaye sasa yuko, aliyekuwa ndani Yake, sasa yuko ndani yetu, pia huihuisha miili yetu ipatikanayo na mauti.” Usiogope, ewe rafiki, M-w-a-n-a amefufuka. Mwana amefufuka. Hakuna . . .

315 Sasa angalia kugeuzwa. Tulikuwa, kila mmoja, tumewakilishwa pale. Kulikuweko na watakatifu walio hai waliokuwa wamenyakuliwa, kulikuweko na Eliya aliyesimama pale; na pale alisimama Musa, wale watakatifu waliokufa . . .? . . . Pia, wote wawili walikuwa na Nguvu za kuhuisha. Kama mmoja alikufa, na huyo mwingine hakufa, wote wako pale.

316 Angalia, loo, angalia kile tunachoona leo katika siku hizi za mwisho. Jambo lile lile aliloahidi Yeye, Yohana 14:12. Sasa angalia. [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] Bila shaka.

Watu husema, “Unadai una nguvu?” La, la, la.

317 Sisi ni kama hao tu kwenye Mlima wa Kugeuzwa, mnaona. Kweli, hatudai nguvu. Lakini, sisi, kama—kama walivyokuwa . . . Kwenye Mlima wa Kugeuzwa, hawakuwa wakisema, Musa, aseme, “Angalieni, angalieni mimi ni nani,” wanafunzi waseme, “angalieni mimi ni nani, angalieni mimi ni nani.” Mnajua kilichotukia? Angalieni, wao walimwona Yesu ametukuzwa. Hilo tu ndilo walilotaka kuona limewakilishwa, Yesu aliyetukuzwa.

318 Basi ndivyo ilivyo leo, hatujaribu kuwa mtu fulani mkubwa. Hatujali yale watu wanasema juu yetu. Jina letu si kitu; ni Jina Lake. Maisha yetu, si kitu; ni Maisha Yake. Ni Nguvu Zake, si nguvu zetu. Na kuna jambo moja tu tunalopenda kufanya, ni kumwona Yeye ametukuzwa. Na jambo hilo linawezekanaje? Wakati Yeye ametukuzwa ndani yetu, kwa kufufuka Kwake ambako kumo ndani yetu. Tunamwona Yeye amewakilishwa tena jinsi alivyokuwa, leo.

319 Mlilipata jambo hilo? Mnaona, shauku yetu si kutukuzwa. Shauku yetu si jina fulani kubwa kubwa. Shauku yetu si

kukuza kanisa fulani, ama kuwapata wengi zaidi katika shule ya Jumapili, ama kujaribu kuingiza, kushurutisha, kusukuma ndani, kuandaa pikiniki, karamu, ama kuleta nishani, watu waungwana, ama kitu kingine kama hicho. Hiyo siyo shauku yetu. Shauku yetu ni kumwona Yeye ametukuzwa. Kutukuzwa, (ati nini?) si kwa majivuno; bali ndani yetu, maishani mwetu, kuthibitisha Yeye yu hai na anaishi ndani yetu.

³²⁰ Kama naweza kujiondoa mwenyewe njiani, ili kwamba wakati William Branham hata hafikiriwi, nawe hata hufikiriwi, mpaka tunapoweza kumwona Yesu ametukuzwa ndani yetu. Kumwona Yeye, hiyo ndiyo shauku yetu. Hilo ni kuhu- . . . linatupa sisi Nguvu za kuhuisha. Na inatupa furaha, kujua ya kwamba sisi tuko pamoja Naye, mwili na mfupa Wake pia, tukiwa Bibi-arusi Wake; na tukiona njia Zake zile zile zilizothibitishwa, zikihakikisha ndani yetu ya kwamba Yeye sasa amefufuka katika wafu. Mnaona?

³²¹ Si ajabu Yeye alisema, “Msiogope,” maana sasa, angalieni, tumekombolewa Naye, na sasa tumefufuka pamoja Naye. Hiyo ndiyo maana ya Pasaka kwa watu, “kufufuka pamoja Naye!” Angalia. Sasa tuna Roho Wake ndani yetu sisi, hati ya kumiliki imelipiwa kabisa.

³²² La, husemi, “Vema, natumaini nitafaulu.” Tayari umefaulu. Si kwamba, “*Nitafaulu.*” Tayari nimefaulu. Mimi sikufaulu; Yeye alifaulu kwa ajili yangu mimi. Mnaona? Si mimi; Yeye! “Vema, Ndugu Branham, wao wanasema. . .” Sijali wanalosema. Pale Yeye alifaulu, kwa ajili yangu. Hilo tu ndilo ninalotaka, ninalojali.

³²³ Mimi tu—mimi ninataka tu kumwona amedhihirishwa. Unawezaje kufanya jambo hilo, kumwita ashuke? La. Yeye yumo ndani yako. Unaona, Yeye yuko ndani yako. “Vema, basi, Bwana, kama naweza kujiondoa njiani, Wewe unaweza kujidhihirisha. Mimi mwenyewe. . . Unawezaje kufanya jambo hilo? Kwa sababu Wewe ulilikusudia namna hiyo. ‘Wote alionipa Baba Yangu watakuja.’” Angalia. Utukufu!

³²⁴ Pamoja na huo ushuhuda wote uliokusanywa, tukiwa nao sasa asubuhi ya leo, loo, ninafikiri juu ya ule wimbo:

Kwenye asubuhi hiyo ya ufufuo,
Wakati kamba za mauti zitakapokatwa,
Tutafufuka, (Haleluya!) tutafufuka!

³²⁵ Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tutafufuka! Katika Yeye tunakuwa sehemu Yake, ile Pasaka, siri ya Mungu iliyofunuliwa kama ilivyokuwa wakati huo, ya Uhai baada ya mauti. Sisi sasa tu hai, tuliokuwa wakati mmoja tumekufa kwa dhambi na makosa. Ule Muhuri wa kweli wa Pasaka umeyavunja mauti yalizonizunguka, nami ni hai. Ile Muhuri ya Pasaka, hapo

mwanzo, ilivunja muhuri ya Kirumi, Muhuri ya Pasaka, ambayo alikuwa ametiwa muhuri kwake. Na watu, walipokufa, walikuwa wamekwisha; bali Yeye aliivunja ile muhuri na kuifunua ile siri. Na sasa Mungu, kwa Roho Wake Mtakatifu, ameivunja muhuri iliyoyafunga maisha yetu, na Kristo amefunuliwa ya kwamba Yeye anaishi ndani yetu, kwa kuwa sasa tumehuishwa pamoja Naye. Loo, ukurasa baada ya ukurasa.

Tutafufuka, (Haleluya!)
 Tutafufuka! (Amina!)
 Kwenye ile asubuhi ya ufufuo,
 Wakati vizuizi vya mauti vitakapovunjwa,
 Tutafufuka, (Haleluya!) tutafufuka!

³²⁶ Loo, hivi hamna furaha! Nina furaha sana! Huko nyuma kabisa, kwenye kibanda kidogo cha makaa asubuhi moja, zile muhuri zilivunjwa, nami nikafufuka pamoja Naye, kiumbe kipya. Nguvu Zake za kuhuisha; Mwana amefufuka.

³²⁷ Si muda mrefu uliopita, nilisimuliwa hadithi ndogo juu ya—ya mvuvi. Jamaa mmoja alikuja akamwajiri mzee mvuvi kumpeleka akavue samaki Pwani ya Magharibi. Wao walitoka wakaenda asubuhi hiyo.

³²⁸ Iwapo mmoja wenu ameshavua samaki mkubwa mwenye nyama nyekundu, basi, unajua linalotukia, kunakuwa na ukungu mwingi sana kule. Ninamwona maskini ndugu yangu, Eddie Byskal, kule chini, mmishenari kwa wahindi kule nje. Nasi tulivua samaki, sisi wenyewe, huko kwenye pwani hizo.

³²⁹ Kwa hiyo mvuvi huyu alikuwa kwa namna fulani mjinga, mwajua. Yeye alienda kuvua samaki, nao wakachukuliwa na mkondo wa maji. Wakingojea kupambazuke, mwajua. Nao—nao wasingesikia honi ya ukungu ikilia tena, naye huyu mvuvi akahangaika sana, akasema, “Aisee, tunachukuliwa na mkondo baharini! Jamani!” Yeye akahangaika sana.

³³⁰ Akasema, “Keti chini, mwanangu. Keti chini.” Huyu Mzee mvuvi, ametulia, mwajua. Alijua alilokuwa anasema. Kasema, “Ngoja tu mpaka jua litakapochochoza, ndipo tutaweza kuona mahali tulipo.”

Unasema, “Ni lazima niwe Mmethodisti? Mbatisti? Mpentekoste?”

³³¹ Ngojeni tu. Mwana akitokea, tutaona mahali tulipo. Yeye ni Neno. Ngojeni mpaka mtakapoona Neno limedhihirishwa, likiangazia ile Mbegu, ule Mganda wa kutikiswa, tutaona tulipo.” Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³³² Samahani niliwaweka muda huu wote. Ni wangapi wenu mtangoja hata usiku wa leo? Loo, basi njoni tu tena, jioni ya leo, mnaona. Yapata saa moja? Ulikuwa na mtu mwingine? [Ndugu Neville anasema, “La.”—Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu.

³³³ Kuna mmoja hapa, ama wengi, ambao hawana Nguvu hii ya kuhuisha ndani yao? Mwana ameangaza kote, nawe umeketi katika maskani hii, umesikiliza kanda, na hata hivyo Roho hajawahi kukuhuisha hata ungeweza kulifuata Neno la Mungu? Laiti ninyi wanawake na ninyi wanaume mngeweza kutii kila Neno ambalo Yeye ameandika! Loo, hilo ni jambo la hatari. Vipi kama ungekuwa mbegu iliyokufa, hamna uhai ndani yako! Bali kuna kitu ndani yako, kinachokwambia, “Na—nataka kuinuka, asubuhi ya leo. Nataka kuinuka kutoka katika hali niliyomo. Sitaki kuwa tu mbegu iliyokufa, kuachwa mavumbini na mbao zilizoachwa pwani na maji. Nataka kuinuka.”

³³⁴ Waweza kuinua mkono wako, useme, “Niombe, ndugu?” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Jamani, angalia hiyo mikono; hakuna njia kamwe kwa ajili ya wito wa madhabahuni. Kile tunachoita wito wa madhabahuni, watu wanakuja wanazunguka madhabahu, mimi siupendi sana, hata hivyo. Jambo hilo liliongezwa tu kanisani katika siku za ufufuo wa Kimethodisti. Mnaona?

³³⁵ Biblia ilisema, “Nao walioamini, mnaona, walibatizwa.” Kuna kidimbwi hapa, kimejaa maji, kikingojea mtu ye yote aliye tayari kufa kwa nafsi yao.

³³⁶ Sasa, waweza ukazikwa, mara nyingi, katika Jina la Bwana Yesu; bali mpaka hiyo Mbegu iwe Uhai, mnaona, haitahuishwa. La, la, la. Ubatizo wa maji ni kama umande ulioshuka kutoka mbinguni; unaweza kuiangukia mbegu, bali, hamna Uhai mle, haiwezi Kuishi.

³³⁷ Bali kama huo ubatizo halisi wa maji, wa kufa kwa nafsi yako, na uko tayari kufa kwa kila kitu ulichowahi kufundishwa na kanuni na madhehebu, ambayo ni kinyume cha Neno, nawe utatembea kama mwana ama binti wa Mungu, nawe unamaanisha jambo hilo moyoni mwako, angalia kile ambacho ubatizo huo wa maji utakufanyia asubuhi ya leo. “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la makosa yenu, dhambi zenu, nanyi mtapokea ule Mganda, sadaka ya kutikiswa. Mtapokea Nguvu za Utendaji, Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa hao wote. Kwa vizazi vyote, itakuwa.

³³⁸ Baba Mungu, ni—nimezungumza kirefu, na kuchukua wakati mwingi wa watu, bali, Bwana Mungu, hakuna kukoma katika jambo hili. Inaonekana tu huna budi kuacha na kuondoka, na kupumzika, kisha kurudi. Tunaishi katika ulimwengu unaokufa, miongoni mwa watu wanaokufa; tukiwa na Ujumbe wa Uzima, pamoja na ushuhuda wa Kufufuka. Mungu mpendwa, tutakuwa na miili ipatikanayo na mauti mara moja tu, na itakuwaje tukiacha nafasi hii itupite?

339 Mioyo yetu inawaka; nafsi zetu zimesisimka; hawa ambao wameingia. Na wengi hapa wanausia Ujumbe huu asubuhi ya leo. Ndio, mia mbili ama mia tatu waliinua mikono yao. Wao wanataka kuamini, Bwana. Loo, hakika hiyo mbegu haijakufa, Bwana. Wangewezaje kuinua mikono yao namna hiyo? Kuna kitu fulani. Ee Mungu, ni ule utu wa kale, ni yule mke wa Ayubu akisimama pale, akisema, “Loo!” Lakini, Bwana, hebu huyo Ayubu, huyo mwamini, aingie, asubuhi ya leo, afe kabisa, na azikwe hapa katika ubatizo huu wa maji.

340 Yale matone ya umande yanayotoka Mbinguni, Neno la Mungu linalosema litasafisha kila dhambi na kuiondolea mbali! Unabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili gani? Ondoleo la dhambi zako, dhambi huondolewa katika Jina la Yesu Kristo.

341 Naomba, basi, Baba, naomba. . . Iwapo wao ni wagonjwa, na waondoke wakiwa na afya. Naomba, iwapo wao ni viwete, na watembe chini ya Nguvu za Roho Mtakatifu. Kama wao wamekuwa wenye dhambi, naomba waondoke wakiwa wamesafishwa na ni wasafi. Na ile mitambo, kwa kuingia; zile Nguvu za Utendaji zitokazo Juu, Roho Mtakatifu, na zije na kuwanyakua, Bwana. Ihuishe miili yao ipatikanayo na mauti, ndipo tutakaposikia lugha mpya halisi, nguvu za Mungu, upendo usioelezeka, neema ifayo na neema iliyo hai; na Kristo aliyefufuka, Mwili, Bibi-arusi akimwakilisha Yeye duniani.

342 Baba, wao ni Wako. Waliinua mikono yao. Nimelihubiri Neno. Sasa, Baba, wapokee, naomba. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba hayo. Amina.

343 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! Yeye si wa ajabu? [“Amina.”] Mmeridhika ya kwamba ninyi ni sehemu ya kufufuka huko kwa Pasaka, ya kwamba mlifufuliwa pamoja Naye? [“Amina.”] Inua mkono wako. Wewe ni sehemu yake.

344 “Watoto wangu wadogo,” kama vile Paulo angalisema. Si kujaribu kumwiga, bali, ule upendo, nawapenda. Mimi hushika njia na cho chote kile, ili kufika hapa, nipate kuzungumza nanyi. Natoka jangwani, kuvuka barafu inayochukuliwa na upepo, na kadhalika, kufika hapa. Tunaruka kwa ndege. Nanyi mnaendesha magari kutoka kote nchini, tupate kukusanyika pamoja. Tunapendana.

345 Sisi ni sehemu ya mmoja kwa mwingine. Msimruhusu Shetani awaambie jambo lingine. Tukiwa sehemu ya mmoja kwa mwingine, sisi ni sehemu Yake. Nasi ni raia pamoja wa ule Ufalme, tukizifurahia baraka hizi, pamoja, za kufufuka.

346 Na sasa, mnaona, sasa tayari mmefufuliwa. Mungu alipomwinua, Yeye alikuinua. Mwana sasa hivi yu juu yako, na sasa unakua kufikia Maisha makamilifu kama alivyokuwa

Yeye, upate kufufuliwa kabisa katika siku hiyo ya mwisho. Una uwezekano wako, ulio nao sasa. Unajua kwa ni nini? Nafsi yako ilibadilishwa, sivyo? Mwili wako ulitiishwa Kwake, sivyo? Ukatiishwa kwa (kitu gani, kanisa fulani?) Neno, ambalo ni Uzima, ndipo sasa umefufuliwa katika wafu. Ni Pasaka, kwangu mimi pamoja na Yesu. Ni Pasaka, kwako wewe pamoja na Yesu. Na ni Pasaka, kwangu, kwangu, pamoja na Yesu. Sisi sote...Ama, Yesu, wewe, na mimi, sote tumefufuliwa pamoja.

347 Nasi tutafufuka katika siku ya mwisho, hata ingawa roho zetu zitaiacha miili yetu, hata ingawa miili itaingia kutu, na huenda ikaingia mavumbini, na ichomwe moto, na iwe kwenye kilindi cha bahari. Biblia ilisema, “Malaika alimwaga yake baharini, na kila kitu kilichokufa kikafufuka.” Hakuna kitu kinachoweza kutuficha, wala kututenga, na Mungu huyo tunayempenda vizuri sana, ambaye ametufufua sisi pamoja.

348 Mungu awabariki. Nimewaweka hapa muda mrefu. Kama hao watu wangali kwenye simu hiyo, wao bila shaka...Kwa senti hamsini kwa dakika moja, wamelipa kwelikweli, asubuhi ya leo. Bali, nisingeweza kabisa kumalizia kwenye saa hiyo, ilinilazimu tu kuendelea.

349 Sasa, Bwana akipenda, nitarudi usiku wa leo, kuzungumza nanyi tena. Na kama siwezi, na halafu ninyi nyote mnajua... Nadhani hatuko kwenye...ama la...Hatuwasiliani kwa simu tena? Hatuwasiliani kwa simu tena.

350 Mnajua mahali ninakoenda, sivyo? Afrika! Nimepiga simu kwa muda mrefu; kwa miaka mingi nimejaribu kurudi. Sasa ono, Roho wa Bwana ameitengeneza njia. Walisema, wakati maskini wananchi hao waliposikia jambo hilo, ya kwamba sikuja wakati wa mwisho nilipokuwa kule, wao walilala sakafuni, mchana na usiku, na kuomboleza na kulia, na kusema, “Bwana, tumefanya nini?” maelfu yao. Watu hao hata hawaamini wana nafsi. Mnaona? Nao walilia wakaomboleza, na wakalia.

351 Msitume neno mapema. Tafadhali msitume. Mnaona, kama ikitokea kwamba hiyo viza ipitie kule na kuingia miongoni mwa wahudumu, wao wangenikatalia papo hapo. Sina budi kwenda kama mwindaji. Ninakwenda kwa yule malkia aliyeleta mabehewa kumi na saba ya gari moshi wakashuka wakaja kwenye mkutano. Nitapanda niende kule na kuwinda katika nchi yake. Basi nikiingia kule, pasi yangu na kila kitu vinaonyesha mwindaji, si ibada ya dini.

352 Halafu kutakuweko na ndugu mmoja atakayekuja kunilaki, aseme, “Mbona usifanye mkutano mdogo kwa ajili yetu?” Viwanja vya mpira tayari vimekodiwa. Wao hata hawajui jambo hilo. Mnaona? Loo, utukufu!

353 Ombeni ya kwamba mapenzi ya Mungu hayatazuiwa. Ya kwamba, nafsi yangu ambayo imeililia Afrika tangu nilipoondoka, naomba niweze kurudi tena, ndipo niwalettee ujumbe wa mkutano mkubwa sana. Labda sitawaona tena, tangu leo, hata nitakaporudi. Tunaelekea, katika siku chache tu sasa, Mei 10. Mtaniombea? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

354 Kumbukeni, hujui shida ni nini, mpaka ufike kule; wachawi kila upande, na pepo, na usifikiri wao hawajui la kufanya. Mnaona? Basi afadhali ujue unalozungumzia, unaposimama mbele yao. "Bali namjua Yeye niliyemwamini, nami nasadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana Kwake hata siku ile."

Sasa, kuna lesa zilizo hapa.

355 Mungu mpenzi, kwa kuwa Ujumbe huu asubuhi ya leo, wa ufufuo, nami nikisimama hapa, Bwana, na kuthibitisha kwa Neno ya kwamba Nguvu hizo za kuhuisha zimo katika mtoto anayeamini. Kwa hiyo, mara nilipoamini, katika imani, ya kwamba Nguvu hizo za kuhuisha zimeyabadilisha maisha yangu. Na watu hawa wanaamini, Bwana, na jambo Hilo lilibadilisha maisha yao. Nasi tunaombeana.

356 Ninaweka mikono yangu juu ya lesa hizi, ili kwamba... Naomba Mungu, Yeye aliyemhuisha Yesu Kristo na kumfufua katika wafu, na Roho huyo aliyemfufua katika wafu, awe anaishi ndani ya mwili wetu.

357 Yule Roho aliyekuwa katika mwili wa Elisha, ambaye, baada ya kufa na hamna kitu ila mifupa, alikuwa na Nguvu za kuhuisha ndani yake. Mikono ya wale mitume ilikuwa na Nguvu za kuhuisha ndani yao. Nia za wale mitume, macho ya wale mitume, ndi—ndimi za waumini, vyote vilikuwa na Nguvu za kuhuisha.

358 Sasa naomba Nguvu hizo za kuhuisha, ninapoliweka Neno hili juu yao, na mikono yangu kuwakilisha mwenye kumiliki, kwa neema, ya Nguvu hizo za kuhuisha, na zihuishe kila mmoja wa miili hii migonjwa, na ipate afya tena, Mungu, katika Jina la Yesu Kristo.


359 Na isiwe tu kwa lesa hizi, bali kwa hao watu huko nje kwenye wasikilizaji, kila mmoja anayeugua. Watoto hao wadogo, watu wazima, hata wawe nini, hizo Nguvu za kuhuisha na ziwahuishe sasa hivi, katika Jina la Yesu. Amina.

360 Sasa, ni wangapi walio na Nguvu za kuhuisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, iwapo hizo Nguvu za kuhuisha zimo ndani yenu.

361 Sasa, kuna kitu kimoja tu cha kuzizuia, kuzipinga, nacho ni kutokuamini kwako. Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, akaponywa; askari wa Kirumi alimtemea mate usoni Mwake,

akaenda kuzimuni. Mnaona? Kwa hiyo ilibidi... inategemea mahali ulipo. Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini jambo hilo?

³⁶² Sasa nataka mwinamishe vichwa vyenu mwombeane. O—ombeni tu mara moja, semeni tu, "Bwana, mtu huyu..." Mnaona, ombeaneni tu.

³⁶³ Mungu mpendwa, tunafanya jambo hili katika Jina la Yesu Kristo, Jina pekee walilopewa wanadamu ambalo kwalo tungeweza kuokolewa ama kuponywa. Watu hawa, ambao ni raia wenzangu wa Ufalme, wenye kumiliki Nguvu za kuhuisha, lihuishe kwao, Bwana, sasa hivi. Naomba Roho aende kutoka tai hadi tai, kutoka kwenye Neno hadi Neno, mpaka utimilifu wa Yesu Kristo udhihirishwe katika kila mmoja wa hiyo miili, kwa ajili ya haja za kimwili, za kiroho, ama haja zo zote walizo nazo, tunapowekeana mikono. Katika Jina la Yesu Kristo. 

Ni Kuchomoza Kwa Jua, Vol. 8 No. 8
(*It Is The Rising Of The Sun*, Vol. 3 No. 12R)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Aprili 18, 1965, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1996 na Voice Of God Recordings.

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

Copyright notice

All rights reserved. This book may be printed on a home printer for personal use or to be given out, free of charge, as a tool to spread the Gospel of Jesus Christ. This book cannot be sold, reproduced on a large scale, posted on any website other than www.branham.org, stored in a retrieval system, translated into other languages, or used for soliciting funds without the express written permission of Voice Of God Recordings®.

For more information or for other available material, please contact:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org